



IMETOSHA

**Wote tukemee
kutekwa,
kuuawa**

Tahariri Uk. 2; Habari Uk. 6,7,8,20&21



Ngorongoro bado wamtaka Samia Uk. 25

Tahariri/Katuni

IMETOSHA! Wote tukemee kutekwa, kuuawa

PAMOJA na kwamba hakuna anayeweza kujitokeza akakiri kwamba ndiye anayeteka na baadaye kuuwa idadi inayoongezeka ya Watanzania wanaopotezwa, lakini jambo moja kubwa lenye uthibitisho ni kwamba matukio haya yanaichafua nchi.

Inasikitisha kwamba matukio ya kutekwa, kufichwa, kupigwa, na wengine kuuawa, yamekuwa yakiripotiwa kila uchao kupitia vyombo vya habari, na hasa mitandao ya kijamii, na kibaya zaidi wanaohusishwa, ni vyombo vya serikali.

Pamoja na kwamba vyombo hivyo vinakanusha kuhusika moja kwa moja, lakini – kwa baadhi ya matukio, bado kitanzi cha lawama kinavifunga, kwani vinamebeba dhamana ya kuhakikisha uhai wa binadamu – tena Watanzania, unalindwa kwa gharama yoyote ile.

Imetokea siyo mara moja ama mbili, watu wakitekwa, wakiteswa na wengine, isiyokuwa bahati kwao, kuuawa kwa mateso makali. Binadamu yeyote akiona picha ama akivuta hisia za wenzetu waliokumbwa na kadhia hii ya ushetani, atahisi uchungu wa kukaribia kifo cha kulazimishwa.

Pambazuko, kama inavyoaminika kuwa kwa Watanzania wengi, lilingwa kwa taharuki baada ya kuthibitika kwa taarifa za kutekwa na hatimaye kuuawa kwa Ali Mohammed Kibao, ambaye alikuwa Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Chama cha

Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kibao, ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Taifa ya Chadema, inaelezwa kuwa Ijumaa ya Septemba 6, mwaka huu, alikuwa akisafiri ndani ya basi la Tashrif na baadaye basi hilo kusi-mamishwa na “watu wasiojulikana” – wakiwa na pingu, ambao walimshusha maeneo ya Tegeta, Dar es Salaam.

Baada ya kumshusha, walionekana kumpakia ndani ya gari aina ya Landcruiser na kuondoka. Hakuonekana tena, hadi jana; Jumapili – Septemba 8, ambapo mwili wake – usiokuwa na uhai, ulipatikana maeneo ya Ununio, Dar es Salaam ukiwa umejaa majeraha makubwa. Kifupi, aliuawa.

Sisi Pambazuko, kama tulivyokemea kutekwa, kuumizwa na pengine kuuawa kwa Watanzania wengine na “watu wasiojulikana,” tunaomba umma wote wa Watanzania kuungana nasi kuikataa hali hii inayoendelea kuota mizizi.

Ilikuwa jana – watu walitekwa, ikawa leo – watu wanatekwa, je, kesho itakuwa zamu ya nani?

Tuamini kuwa hakuna ardhi iliyoshibishwa damu za binadamu, zilizomwagwa kwa nguvu ya yeyote, ikamea amani, ustawi na hata maendeleo.

Tusikae kimya; wote tuseme IMETOSHA SASA. Tusitekwe. Tusiuawe kwa sababu iwayo yote.



Dkt. Mpango kanisani Arusha...



Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango (kushoto), akiwa na viongozi wa Kanisa la New Life Outreach Tanzania wakati wa kilele cha Sherehe za Maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 50 ya kanisa hilo iliyofanyika katika eneo la Sakina, Arusha juzi. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



China kukopesha trilioni 138/- kwa Afrika



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Watanzania wanaoishi China Jijini Beijing mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu)

Na Andrew MSECHU

NCHI za Afrika zimehakikishiwa kupata mikopo inayofikia shilingi trilioni 138 (karibu Yuan bilioni 360), itakayotolewa na China ikiwa ni mikopo nafuu katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Hatua hiyo ni moja ya maazimio yaliyojiri katika mkutano wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (Focac), uliomalizika Alhamisi iliyopita, Septemba 5, 2024.

Katika mkutano huo, Rais Samia ambaye alipata nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya nchi za Afrika Mashariki, alisema wamekutana ikiwa ni sehemu ya kusherehekea urafiki baina ya China na Afrika ambao umekuwa wa manufaa kwa maisha na maendeleo ya watu wao katika nyanja za uchumi na sekta ya miundombinu.

“Ukiacha changamoto za kiuchumi zilizosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, China imeendelea kuhakikisha inatimiza ahadi zake zilizotolewa awali kupitia mikutano ya Focac katika kuhakikisha kuwa tunatimiza malengo muhimu ya maendeleo yetu...”

“Matokeo ya ushirikiano yako wazi kwenye uchumi wetu na hii inadhihirisha kuwa China ni rafiki wa

kweli kwenye vita yetu dhidi ya umaskini na kuimarisha uhusiano huu China inadhihirisha ushiriki wake katika kuchochea uimarishaji miundombinu, ukuaji wa kasi wa viwanda na uboreshaji wa sekta ya wazalishaji wa kati na wadogo katika nchi zetu,” alisema Rais Samia.

Alisema miaka ya hivi karibuni dunia ime-shuhudia ukuaji wa kasi wa biashara na uwekezaji baina ya China na nchi za Afrika kama ambavyo imekuwa ikibainishwa kwenye mkutano huo wa Focac.

Rais Samia alisema Tanzania ni mfano wa kuigwa kwenye masuala yanayohusu uibuaji wa fursa za kijamii na kiuchumi kutoka China.

Ukarabati wa Tazara

Pembeni ya mkutano huo wa Focac, Rais samia, Rais Hakainde Hichilema wa Zambia na mwenyeji wao, Rais wa China, Xi Jinping, walishuhudia kutiwa saini makubaliano ya kukarabati kilometa 1,860 za Reli ya Tazara, ikiwa sehemu ya kampeni za kuboresha usafiri wa reli na bahari katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Februari mwaka huu, China ilipendekeza kukarabati reli hiyo kwa gharama ya dola bilioni moja (karibu shilingi trilioni 2.6).

Makubaliano hayo yanatiwa saini muda mfupi baada ya mapema mwaka huu, Benki ya Dunia kuidhinisha ufadhili wa dola milioni 270 (karibu shilingi bilioni 702) kusaidia kuboresha usafiri kati ya Tanzania na Zambia na kuimarisha biashara ya kikanda.

Dkt. Kahyoza

Mchumi na mchambuzi wa masuala ya siasa, Dkt. Bravious Kahyoza, amesema kwa ujumla, wakati Tanzania wakipokea msaada huo, bado Afrika haijawa na mikakati mizuri ya kujenga viwanda na kuchakata rasilimali za kiuchumi, na kushangaa kwanini bado bara hilo linasafirisha rasilimali za kiasili.

“Kwa kweli hili ni jitihada nzuri kwamba marais wa Zambia na Tanzania wametafuta namna ya kuhuisha uhai wa reli ya Tazara, lakini ukiangalia kwa ujumla, barani Afrika, eneo hili la usafirishaji wa bidhaa kuelekea China bado kuna maswali mengi...”

“Kwa mfano, kati ya mwaka 2012 hadi mwaka 2022, thamani ya madini yanayotoka Afrika kwenda China imeongezeka kutoka dola bilioni 15 hadi dola bilioni 60 ndani ya kipindi kama cha miaka 12 hivi...”

Inaendelea Uk. 23

Ajiapiza kuteka mtoto wa anayetuma kuteka watu

Na Igo Al

TANGAZO lilisambazwa juzi jioni kwamba Mtanzania, raia wa makamo ambaye ana sifa moja kubwa; ya kusema ukweli daima, jana angekuwa na mkutano na wanahabari nyumbani kwake, Kijitonyama, Dar es Salaam.

Pamoja na kwamba tangazo hilo lilieleza kuwa mkutano huo ungeanza saa 5:30 asubuhi, lakini waandishi hao waliwahi kufika, kwani wamekuwa wakiamini, raia huyo, anayeitwa Mzee Tai, ana “stori” za maana kila anapowaita.

Kwa kuwa wanahabari waliwahi, Mzee Tai hakuona sababu ya kuendelea kujifungia chumbani kwake, bali aliamua kutoka mapema, saa 4:05 asubuhi na kujongea alipoandaa kukutana na wapasha habari hao.

Akiwa amevalia tisheti yake maarufu; ya rangi ya kijani, yenye picha na mwanamke mwenye ushungi na miwani mikubwa na mipana, ikiwa imeandikwa; “mitano tena kwa Mama” – Mzee Tai alianza kwa kuwashukuru waandishi waliofika kwa kuitikia mwito.

Bila kupoteza muda, Mzee Tai alieleza sababu za kuomba kukutana na kuzungumza na wanahabari hao. Alisema kuwa ana jambo muhimu la kuiponya nchi.

“Nimewaita hapa kuwaeleza kwamba niko tayari kuiponya nchi sasa, baada ya kukaa na kutafakari sana kuhusu janga la kuteka watu na wengine kuuawa bila sababu,” alisema Mzee Tai.

Akaendelea; “Nimesikia watu wengi sana wametekwa, lakini ni kama hakuna mwenye kutambua dawa ya kukomesha utekaji huu, ambao kimsingi, ni ushamba tu na ujinga.”

Mzee Tai akawauliza wanahabari hao, endapo miongoni mwao alikuwepo mwenye kutambua dawa ya kukomesha utekaji na mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

Mwanahabari mmoja, akasimama na kueleza kuwa yeye anadhani wenye uwezo wa kumaliza


janga la utekaji na kuua watu wasiokuwa na hatia ni Jeshi la Polisi.

Baada ya jibu hilo, Mzee Tai akaonekana kukunja ndita, akamtazama mwanahabari yule kwa jicho kali na kufungua mdomo wake akasema; “kaa chini wewe, unasema nini?”

Mwanahabari yule, hakujibu lolote, ndipo Mzee Tai akasema; “nyie sijui mmerogwa na nani, mnashindwa hata kuchunguza wasiojulikana ni kina nani? Mnafanya kazi gani sasa.”

“Mimi dawa ya kumaliza utekaji, ninayo. Ni kumteka mtoto wa anayewatuma watekaji kuteka watu. Na nitakwenda kuteka, Msiniulize ni mtoto wa nani na wala nitampataje.”

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Yaelekea kuwa mazoea kuteka, kuua



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam jana. (Picha na Chadema)

Na Mwandishi WETU

KUTEKWA na hatimaye kuuawa kwa Ali Mohammed Kibao, ndani ya saa 27, kumeongeza idadi ya Watanzania wanaoteswa na kukatizwa uhai wao.

Maoni ya Watanzania wengi, ni kwamba hili ni doa ambalo linapaswa kupigiwa kelele na kila mpenda haki ili kukomeshwa kwa utaratibu huu wa kuteka na kuua unaofanywa na wale wanaotajwa kuwa ni “watu wasiojulikana.”

Kibao, ambaye ni Mjumbe wa Sekretarieti ya Taifa ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), anaongeza idadi ya Watanzania ambao wametekwa, kuumizwa na wengine, isiyokuwa bahati kwao, kuuawa.

Pambazuko limedokezwa na vyanzo vya habari kuwa wapo wanaouawa na kupatikana na wengine miili yao kutupwa baharini, kuzikwa kusikojulikana ama kutelekezwa porini ambako huliwa na wanyama wakali.

Vyanzo kadhaa vya habari vimelieleza Pambazuko kwamba Kibao alitekwa ndani ya basi la abiria la Tashrif Ijumaa – Septemba 6, na kushushwa kwa nguvu na watu waliobeba silaha za kivita, kumpakiza kwenye gari aina ya Land-cruiser na kutokomea naye.

Inaelezwa kuwa baada ya kumpakia mzee huyo, anayekadiriwa kuwa na miaka zaidi ya 70, gari hilo lililombeba, liligeuza na kuelekea Mwenge – likipita Barabara ya Bagamoyo.

Baadhi ya abiria waliokuwa ndani ya basi hilo wameeleza kuwa Kibao alishushwa kwa nguvu na watu waliojitambulisha kuwa ni askari na kwamba walidai “wana shida naye,” hivyo abiria kushindwa kuhoji.

Pambazuko limeleezwa kwamba watu hao walimfunga pingu kabla ya kumshusha, hatua ambayo iliongeza “utulivu” kwa abiria waliokuwamo ndani ya basi hilo kwamba huenda kweli hao waliomchukua walikuwa ni askari.

Imebainika kuwa baada ya kushushwa, basi liliendelea na safari na hakukuwa na “habari” tena za abiria wa basi hilo aliyeshushwa kabla hajafika anakokwenda kama tiketi inavyoonyesha. Basi lilikuwa likitoka Dar es Salaam kuelekea Tanga.

Rais Samia akemea

Baada ya kupokea taarifa za kutekwa na kuuawa kwa Ali Mohammed Kibao, Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia ukurasa wake wa X (zamani Twitter), alieleza kusikitishwa kwa mauaji hayo.

Ameandika: “Kwa masikitiko makubwa nimepokea taarifa ya mauaji ya kiongozi wa Chadema Bwana Mohamed Ali Kibao. Natoa pole kwa viongozi wa chama hicho, familia ya Mzee Kibao, ndugu, jamaa na marafiki.”

“Nimeagiza vyombo vya uchunguzi kuniletea taarifa ya kina kuhusu tukio hili baya kabisa na mengine ya namna hii haraka...”

“Nchi yetu ni ya kidemokrasia na kila raia ana haki ya kuishi. Serikali ninayoiongoza haivumilii vitendo vya kikatili vya namna hii.”

Lawama kwa Polisi

Vyombo vya usalama nchini, hususani Jeshi la Polisi, haviwezi kukwepa lawama ya ongezeko la wimbi la utekaji na kuuawa kwa raia, kwa kuwa ndivyo vinatakiwa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Yaelekea kuwa mazoea kuteka, kuua

Inatoka Uk. 6

Hivyo vimetakiwa kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na hali hiyo na kisha kuu-julisha umma kinachofanyika kukabiliana nayo kama njia ya kupunguza tuhuma kuwa jeshi hilo linahusika kutekeleza vitendo hivyo.

Katika miezi ya karibuni kumeibuka wimbi kubwa la watu kutekwa na kupotea, huku baadhi yao wakipatikana wakiwa wameteswa na kutelekezwa.

Ingawa Jeshi la Polisi limekana kuhusika na matukio hayo kama baadhi ya watu wana-vyotuhumu, lakini ukweli ni kuwa jeshi hilo linawajibika kutoa maelezo kwa kila tukio la utekaji kwa sababu lina wajibu huo.

Watu kadhaa waliozungumza na Pambazuko wakiwamo wanasiasa, wanataaluma, wana-harakati na wananchi wa kawaida, wamelaani matukio hayo ya kiharamia na kulitaka jeshi hilo kuchukua hatua madhubuti kukabiliana nayo.

Mwanasiasa na mwanadiplomasia, Dkt. Willibrod Slaa, amesema ushauri uliotolewa na Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kulifanyia marekebisha Jeshi la Polisi ufanyiwe kazi sasa.

Dkt. Slaa amesema Jeshi la Polisi haliwezi kukwepa lawama kwenye tuhuma za utekaji kwa sababu baadhi ya waliopotea akiwamo Mwenyekiti wa Vijana Chadema Wilaya ya Tememe, Deusdedit Soka na wenzake, walipotea baada ya kuitikia wito wa jeshi hilo.

“Jeshi la Polisi kwa sasa halikarabatiki, livunjwe na kuundwa upya. Rais Samia alikwishape-wa ushauri na Tume ya Haki Jinai aliyoiunda mwenyewe, anasubiri Mungu aje kumshauri?” alihoji Dkt. Slaa.



Viongozi mbalimbali waliojitokeza katika Hospitali ya Mwananyamala wakati wa kukagua mwili wa marehemu Ali Kibao. (Picha na Mtandao)

Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, amependekeza kuundwa kwa tume mahsusi itakayoliangalia suala la utekaji kwa kina na kuja na majawabu yatakayoliwezesha taifa kukabiliana na hali hiyo.

“Hii haitakuwa mara ya kwanza. Huko nyuma tume nyingi zimeshawahi kuundwa, mathalan, ile ya kuchunguza mauaji ya vikongwe, na zikaja na majawabu,” amesisitiza Mwabukusi.


Mchungaji wa Kanisa la Maombezi (GRC) lililopo Ubungo Kibangu, Dar es Salaam, Mchungaji Anthony Lusekelo maarufu kama ‘Mzee wa Upako,’ ameonyesha wasiwasi kuwa kuna watu wanatafuta majibu rahisi katika suala zito la utekaji.

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, Mchungaji Lusekelo alihoji kwa nini suala la waganga wa kienyeji kudaiwa kuhusika na vifo vya watu kadhaa limeibuka wakati huu nchi ikiwa imegubikwa na wimbi la utekaji wa watu?

Inaendelea Uk. 8



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Habari Kuu

Yaelekea kuwa mazoea kuteka, kuua

Inatoka Uk. 7

Alisema inashangaza pia kuona watu ambao wanahoji masuala ya kawaida wanakumbwa na visa vya kupotea kama ilivyotokea kwa Shadrak Chaula wa Rungwe mkoani Mbeya, ambaye alipotea siku chache baada ya kutuhumiwa kucho-ma picha ya Rais Samia aliyokuwa ameichora mwenyewe.

“Mbona picha ya rais inawekwa magazetini na tunayatumia kufungia vitumbua na maanda-zi na hakuna anayetekwa?”

“Hawa wanaovizia na kuteka vijana kwa nini hawateki mafisadi waliojaa serikalini?” alihoji.

Mchungaji huyo akaongeza; “Haiwezekani kijana aandike kwenye mtandao akisema siikubali CCM (Chama Cha Mapinduzi), matokeo yake unasikia kapotea, katekwa.”

“Sheria zipo, kama mtu amekosea mpeleke-ni mahakamani na nchi itatulia, lakini ukifanya vile hata mawazo mazuri utayakosa, mtu ataona nikisema hivi au vile nitatekwa, hii inaleta taha-ruki kwenye nchi.”

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maas-kofu na Mashehe - ya Haki, Amani na Maadi-

li kwa Jamii ya Madhehebu, Askofu William Mwamalanga, ameleleza Pambazuko kuwa ute-kaji ni zao la wasiojulikana ambalo liliasisiwa na utawala wa awamu ya tano.

Amesema kundi hili lilitumika pia kupora fedha za wafanyabiashara na kufunga akaunti zao za benki.

“Katika hili hakuna mtu ambaye yupo sala-ma hata kwa watekaji wenyewe, viongozi wa ki-siasa, rais, mawaziri, wabunge na hata viongozi wa dini. Matukio haya yanaweza kutoa nafasi kwa maadui wa nje kujipenyeza ndani ya nchi yetu na kufanya matukio ya kiharamia,” amese-ma Askofu Mwamalanga.

Jeshi la Polisi liseme

Rais wa TLS, Mwabukusi amesema ukimya wa Jeshi la Polisi ndiyo unazidisha sintofahamu ya matukio hayo ya utekaji wa watu nchini.

“Jeshi la Polisi wanapo mahali pa kuanzia kubaini watekaji kwa sababu baadhi ya vijana waliotekwa na baadaye kupatikana maeneo to-fauti, wapo hai na walieleza wazi kwamba wa-liwahi kufikishwa vituo vya Polisi na baadaye kutelekezwa kwenye maeneo tofauti...”

“Kijana Sativa (Edgar Mwakabela), huyu ali-chukuliwa na askari polisi eneo la Ubungo hadi Kituo cha Polisi Oysterbay, Dar es Salaam, la-kini baadaye alikutwa amepigwa risasi na kut-upwa porini Katavi, mpaka sasa hatujaelezwa ni nani walifanya tukio hili, ni nani amewajibika au kuwajibishwa?” alihoji Mwabukusi.

Amesema masuala ambayo baadhi ya watu waliotekwa wanayahoji siyo mapya, kwani hata kipindi cha uongozi wa

Mwalimu Julius Nyerere (Rais wa Kwanza wa Tanzania), kulikuwa na kipindi kilichokuwa kinarushwa na Redio Tanzania (RTD) wakati huo kikiitwa ‘Mikingamo’ kilichokuwa kinatoa fursa kwa watu kutoa kero zao, sasa iweje leo waonekane wahaini na watekwe?

“Watu walitoa maoni kwa kupiga simu na kuandika barua za kero katika maeneo yao. Hizo kero zilisomwa redioni na hatua zilichukuliwa na serikali ya Mwalimu Nyerere. Sasa hivi watu wanatumia mitandao ya kijamii kuwasilisha kero zile zile kama enzi za Mwalimu, kwa nini hawa watekwe?” alihoji.



Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



China marafiki zetu, 'tuwamulike' vizuri



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na baadhi ya Watanzania wanaoishi China baada ya kuzungumza nao Jijini Beijing mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu)

WIKI iliyopita, China ilifanya mkutano mkubwa kati yake na nchi za Afrika, ukiwa ni sehemu ya juhudi zake za kuimarisha uhusiano na bara hilo.

Mkutano huu ulijumuisha viongozi wa nchi mbalimbali za Kiafrika, akiwemo Rais Samia Suluhu wa Tanzania.

Safu hii leo, inaangalia kwa kifupi fursa na changamoto katika uhusiano huo, mkazo ukiwa kwa nchi yetu na faida zinazopatikana.

Faida za uhusiano wa China-Afrika ni pamoja na mambo yafuatayo;

Uwekezaji wa Miundombinu; China imekuwa ikiwekeza sana katika miradi ya miundombinu Afrika, ikiwemo barabara, reli, na bandari. Kwa Tanzania, reli ya Tazara inabaki kuwa moja ya faida muhimu zaidi za uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Msaada wa kiuchumi; nchi nyingi za Afrika, Tanzania ikiwemo, zimepokea mikopo na misaada ya kiuchumi kutoka China, ambayo imesaidia kuendeleza sekta mbalimbali.

Uhamisho wa teknolojia; ushirikiano na China umewezesha nchi za Afrika kupata teknolojia mpya, hususan katika sekta za mawasiliano na

nishati.

Fursa za biashara; soko la China limetoa fursa mpya za biashara kwa bidhaa za Kiafrika, ikiwemo mazao ya kilimo na madini.

Pamoja na faida hizo, lakini pia kwenye ushirikiano hau, kuna changamoto ambazo zinabidi kutazamwa na kueukwa, endapo inawezekana kufanya hivyo.

Miongoni mwa changamoto hizo ni madeni; mikopo kutoka China imesababisha ongezeko la madeni kwa nchi nyingi za Afrika, ikiwa ni pamoja na Tanzania.

Pia ushirikiano wa China na Afrika ni kama unachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa viwanda vya ndani vya nchi masikini.

Kitu kingine ni kukomaa kwa utegemezi. Kuna wasiwasi kuwa nchi za Afrika zinaweza kuwa tegemezi sana kwa China kiuchumi na kisiasa.

Aidha, masuala ya mazingira nayo yamekuwa yakizungumzwa kuwa China haina urafiki sana na mazingira, hasa kwa nchi za Afrika. Miradi mingi ya China imekuwa ikishutumiwa kwa kukiuka masharti ya kutunza mazingira.

Kwa muktadha wa Tanzania, kama nchi nyingine za Afrika, imepata faida na changamoto kutokana na uhusiano wake na China.

Uwekezaji katika miundombinu, kama vile mradi wa reli ya kisasa, umeboresha usafiri na biashara. Hata hivyo, Tanzania pia inakabiliwa na changamoto za madeni na ushindani wa bidhaa za China katika soko la ndani.

Ili kuhakikisha uhusiano wenye manufaa zaidi, Tanzania na nchi nyingine za Afrika, zinahitaji kuwa makini katika majadiliano na China, kuhakikisha mikataba inayoingia inalinda maslahi ya nchi zao, na kutafuta njia za kupunguza utegemezi mkubwa kwa nchi moja.

Kwa ujumla, uhusiano kati ya China na Afrika una fursa nyingi, lakini unahitaji usimamizi mzuri na uangalifu ili kuhakikisha maendeleo endelevu kwa nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania.

https://instagram.com/evarist_chahali



Tafakuri ya Bagonza

Aliyemteka Soka, eti kaiteka Polisi

Na Dkt. Benson BAGONZA

KUTEKWA kwa Deusdedit Soka na wenzake, kumepigiwa kelele sana.

Hata 'mabubu' waandamizi, wameanza kusema. Mama yangu mzazi Profesa Dorothea (miaka 86 sasa), jana ameniita kwa dharula na kuni-onya, "usiwe unatoka nje usiku peke yako. Hata chooni tafuta mtu akusindikize." Nikamwuliza kwa nini? Akajibu, "walioteka Soka watakuteka".

Nani kamteka Deusdedit Soka? Nina nadharia tano hapa za kutafakari;

Mosi, katekwa na Polisi ili kuwatisha waropokaji. Polisi wamepelekwa mahakamani. Wamekana na kushinda kesi. Wako huru. Hawajamteka.

Pili, katekwa na Chadema ili kusingizia Jeshi la Polisi. Siku zimekuwa nyingi; polisi hawaogopi kusingiziwa. Umma unaamini ni polisi.

Kwamba Chadema wakimpoteza Soka moja kwa moja, itakula kwa Polisi. Polisi wakishindwa kumwkoa Soka kutoka mikononi mwa Chade-

ma, itakula kwao. Mpira uko eneo la goli la Polisi.

Tatu, ametekwa na wajanja wanaotumia jina la Polisi (Rogues). Kutokamatwa kwao ni hatari kwa kila mtu na kila taasisi. Wakiishazoea watateka viongozi wetu na kusababisha hali ya hatari.

Ileweke kuwa watekaji wasiokamatika, ni sawa na silaha moja kupotea kutoka ghala la silaha. Polisi wako lawamani katika nadharia hii.

Nne, Soka na wenzake wamejiteka ili Polisi na chama cha watani wa jadi walaumiwe - CCM. Kazi mojawapo ya Polisi ni kufichua waliojiteka.

Ukijiteka, ukafanikiwa kutokamatwa, wanaolaumiwa ni polisi. Sifa moja ya Polisi na serikali ni kuwa na mkono mrefu. Sasa nani kaukata ukawa mfupi usimkamate Soka aliyejiteka?

Tano, Soka ametekwa na chama cha watani wa jadi wa Chadema kwa sababu Soka ni Chadema. Kwa kuwa kuna mzimu "unawaroposha" wanachama wa chama hicho kukiri utekaji,

Upo ushahidi wa mazingira kwamba Polisi hutumia waropokaji kuisaidia kufanya kazi zake. Asipopatikana siyo kosa la chama kilichoteka. Ni kosa la taasisi inayojihusisha na kuzuia utekaji. Bado Polisi hawajachomoka. Niwasaidieje?

Mpaka hapa, naweza kusema, aliyemteka Soka na wenzake, ameiteka Polisi, maana nadharia nne kati ya tano, zinagota kwa Polisi. Nani aikomboa Polisi kutoka mikono ya watekaji?

Tumewahi kuuona mkono mrefu wa Polisi ukiwa kazini. Majuzi tu, ndani ya saa 24, walio-muua binti Asimwe mwenye ualbino walikamatwa.

Tumesikia habari za mganga wa kienyeji aliyezika watu. Tunaogopa tusijeambiwa aki-na Soka wako humo. Kwamba walienda kupiga ramli chonganishi ya kuwaroga watani waweze kufichua siri za sirini.

Kusitasita kutoa taarifa za uchunguzi wa watekaji ni kutuandaa kutekwa kiroho.

Imetosha sasa, Soka na wenzake waachiwe na nyie watekaji msitekane tena.



Jeshi la Polisi limeimarisha usalama kila kona ya nchi, kutokana na tetesi za kufanyika maandamano ya Aprili 26, 2020. (Picha na Pars Today)

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTagaluka

Viongozi wa dini wakemea kauli dhalili

KAULI za baadhi ya wanasiasa zinazopinga uwepo na uwezo wa Mungu katika kuamua mambo yao, ni za hatari.

Kiongozi wa chama kusema kuwa ushindi wa chama chake hauko chini ya mapenzi ya Mungu, bali ni lazima, ni dhahiri kwamba kuna kupuuza na kukengeuka kwa kada huyo anayesahau hata Nguvu za Mungu.

“Makatibu tawi mpaka leo hii tarehe tatu, bado siku 20 hakuna kitu au siyo? mipango yenu ni nini kuifanya CCM ifanye nini, kwa sababu ushindi wa CCM, hauna Mungu akipenda, hili mnalijua?

“Hee, ushindi wa CCM hauna mpaka Mungu apendee. aah!, Mungu akijaalia, aah! ushindi wa CCM ni nini? ni lazimaa na kushinda ni? Lazimaa hata iweje, kwa hiyo, siyo Mungu akipenda. hee kushinda ni lazima na hakuna Mungu akipenda...”, amesema kiongozi mmoja mwana mama wa CCM ambaye picha yake ya mjongeo inasambaa mitandaoni.

Najua kauli hii hakutoa leo, jana au mwaka huu, aliitoa katika uchaguzi mkuu uliopita ingawa bado inaishi hadi leo, na kwa kuwa haikukemewa kuanzia na viongozi wenyewe wa CCM mpaka viongozi wa dini, kumejitokeza viongozi wengine wamekuja na kauli kama hizi bila kujali athari zinazoweza kujitokeza.

Mathalan, hivi karibuni Watanzania wame-shuhudia kupitia picha mjongeo inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonesha Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Kilwa, Lindi Mustafa Engema akiropoka maneno magumu na mazito kuyasadiki.

“Kwenye wilaya hii, kwa jemedari Mbaruku na Said Timami na Engema tuliobeba dhama-na, nakuthibitishieni heri afe mtu kuliko kutupa ushindi wa CCM. Na siku zote tunaposema huwa tunamaanisha, kwenye kutafuta dola hatuwezi kuchekeana, wala hakuna Uislamu wala Ukristo. Jambo letu ni moja tu, ni ushindi wa CCM.



Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi wakiwa kwenye moja ya mikutano yao . (Picha na Mtandao)

“Na siku zote ninaposema namaanisha, uwongo kweli? (wanaitikia, kweliii) wako viongozi kwenye chama chetu cha mapinduzi, muda wenu unakwisha na mnataka kuondoka. Ninakuapieni wengine sisi hatuendi peponi kwa ajili ya CCM. Tumekataa. Mimi mtu wa moto kwa ajili ya chama hiki...”, anasema Engema bila hofu.

Lakini tumeona Engema, akikiri kuwa haoni haja ya pepo na kwamba, katika uchaguzi, CCM inapaswa kushinda kwa gharama yoyote, hata kama ni kutoa uhai wa mtu.

Kwamba kwa kauli hii inaonesha mtazamo wa kiongozi kuhusu nguvu za kidemokrasia na ushawishi wa chama chake kuliko kuachilia mambo kwa mapenzi ya Mungu.

Kwa upande wao viongozi wa kidini wana-weza kukemea kauli hii kwa sababu inakosa hes-hima kwa maadili ya kidini na inaweza kuathiri umoja wa kidini katika jamii.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Na Godwin CHILEWA,
Houston

Kurunzi la Intelijensia

Polisi haiwezi kukwepa tuhuma za utekaji



Vitendo vya utekaji

HIVI karibuni, tuhuma za utekaji nyara na mauaji ya watu wasio na hatia, zimekuwa kama jambo la kawaida.

Kila unapofungua gazeti au kutembelea mitandao ya kijamii, utakutana na vilio vya ndugu na marafiki waliopoteza wapendwa wao, au kelele za wanaharakati wanaotetea haki za binadamu wakidai kurejeshwa kwa watu wanaodaiwa kutekwa nyara.

Inasemekana kuwa zaidi ya watu 200 wameitekwa nyara au kupotea katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kutokana na matukio hayo, wanasiasa na wanaharakati wameilaumu serikali, hususan Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), kwa kuhusika na utekaji nyara huo.

Hata hivyo, lawama hizo zimekanushwa vikali na viongozi wa serikali, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Jeshi la Polisi.

Pengine utajiuliza kwa nini wananchi wanahusisha vyombo vya dola, hasa Jeshi la Polisi, na utekaji nyara unaoendelea?

Kuna mambo kadhaa yanayoweza kuwa sa-

babu ya lawama hizo, lakini hapa nitazungumzia mambo matatu tu. Kwanza, ni tabia ya ukatili na unyanyasaji unaofanywa na baadhi ya askari wa jeshi hilo.

Ingawa askari wengi wa sasa ni waadilifu na wenye weledi, kundi dogo la askari wakorofi, li-naathiri sana sifa na uaminifu wa jeshi letu.

Askari hao hutumiwa na watu wenye fedha kuwatisha, kuwatesa, kulipiza kisasi, au kuwaadhibu mahasimu wao.

Baadhi ya askari hawa hata hujivunia kutumia maneno kama “nitakuua” au “nitakupoteza” bila kujali athari zake.

Jambo la pili, ni matumizi mabaya ya mam-laka na viongozi wa serikali, hasa wakuu wa wilaya na mikoa; kutoa maagizo kwa askari kukamata au kutesa wapinzani wa kisiasa na watu wasio na hatia.

Hili limethibitishwa na matukio ya awali yaliyofanywa na waliokuwa viongozi wakati wa Rais John Magufuli. Historia haifutiki kirahisi.

Jambo la tatu, ni utaratibu mbovu wa jeshi hilo kuwaruhusu askari waliovaa kiraia kubeba hadharani silaha kubwa.

Kawaida, silaha kubwa kama bunduki, zinapaswa kubebwa na askari aliyevaa sare rasmi za jeshi. Askari yeyote aliyevaa kiraia anatakiwa kubeba silaha ndogo (pistol) na kuificha chini ya mavazi yake.

Utaratibu huu husaidia wananchi kuwa na uhakika kwamba mtu mwenye silaha ni askari, huku ukimpa askari aliyevaa kiraia fursa ya kujipenyeza kwa adui bila kujulikana.

Askari waliovaa kiraia wakiwa na silaha kubwa hadharani wanajitambulisha wazi na hivyo kujikuta katika hatari ya kudhaniwa kuwa ni majambazi.

Ndiyo maana katika nchi zilizoendelea – hasa Marekani, polisi au maofisa wa FBI wanapokuwa na silaha huku wakiwa wamevaa kiraia, hufuata utaratibu ufuatao; kuvaa beji inayotambulisha kazi yao; kuvaa fulana au vest iliyoandikwa POLICE au FBI; na kuning'iniza kitambulisho shingoni.

Mwandishi ni mchambuzi wa masuala ya intelijensia, na mwandishi wa vitabu. Anaishi Houston, Texas, Marekani.

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba



Nguvu ya jamii ‘yakomelea’ sheria rushwa ya ngono



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Mhagama, akifafanua jambo wakati wa kikao cha kamati hiyo kilichofanyika Bungeni Jijini Dodoma. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

JUMA lililoanza Septemba 2, 2024 - lilianza kwa shangwe kwa wanamtandao wa kupambana na rushwa ya ngono hapa nchini.

Chanzo cha shangwe hiyo ni pale Bunge la Tanzania lilipokataa kupitisha kifungu kilichokuwa kimepelekwa bungeni kwa nia ya kukifanyia marekebisho kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Kifungu hicho kinahusu utofauti uliopo kati ya rushwa kwa jumla wake na rushwa ya ngono. Uwepo wa kifungu hicho katika hiyo sheria ulitokana na mchango mkubwa wa Chama cha Majaji Wanawake (Tawja), ambapo tafsiri iliyowekwa ilibainisha kuwa rushwa ya ngono inawahusisha watu wenye mamlaka kutumia vibaya mamlaka yao kwa kudai ngono ikiwa ni sharti la kumpatia mtu haki na stahiki zake au kumpendelea yule ambaye hastahili.

Muswada ulipelekwa bungeni kutaka kifungu hicho kifanyiwe mabadiliko ili anayedai rushwa ya ngono, ambaye ndiye mtu mwenye mamlaka, pamoja na mwathirika, wote waweze kupatiwa

adhabu kwa mantiki kuwa aliyeomba na aliyetoa rushwa na ngono wote wametenda kosa.

Kifungu cha muswada huo namba 10(b) ndicho kilichokuja na marekebisho hayo. Wanamtandao na wapenda haki wote waliinuka na kufuatilia suala hilo kwa kuwa ilionekana kuwa faida iliyokuwa imepatikana kwa uwepo wa kifungu cha 25 sasa, itapotea na tutarejea kule ambapo waathirika wa rushwa na ngono hawataweza kutoa taarifa wanapokutana na madhila hayo, kwa hofu ya kutiwa hatiani na kuadhibiwa.

Suala hili la rushwa ya ngono limewaumiza wengi walio chini ya mamlaka ya walimu, wahadhiri, viongozi kazini, viongozi wa dini na wengineo wengi, kwa kujikuta wamelazimika kutoa rushwa hiyo ili wapate kitu fulani huku wale waliokataa kutoa rushwa hiyo wakipata madhila kama vile kufelishwa mitihani, kukosa au kufukuzwa kazi n.k.

Rushwa ya ngono ni ya udhalilishaji kwa muathirika, inampoka utu wake, inamnyima fursa ya kujiinua na humuweka katika nafasi ya kuwa dhalili au mtumwa kwa muomba rushwa.

Wanamtandao kote nchini kuanzia ngazi ya taifa hadi chini kabisa walipaza sauti kukataa mabadiliko hayo. Walihoji mabadiliko hayo yanafanyika kwa manufaa ya nani?

Walifanya vikao, mikutano na vyombo vya habari, mikutano na kamati husika ya Bunge la Tanzania na hata kuwasiliana na mbunge mmoja mmoja wakitahadharisha ubaya wa mabadiliko hayo kwa taifa na katika kupambana na rushwa ya ngono.

Kilichofurahisha zaidi ni pale Bunge la Tanzania ‘lilipojiongeza’ na kupanua wigo wa ukomo wa adhabu kwa waomba rushwa ya ngono kutoka miaka mitatu jela hadi miaka kumi na faini kutoka shilingi milioni tano hadi milioni 10

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Bunge labaini madudu kwenye sheria ndogo

Na Helen NGOROMERA

KAMATI ya Bunge ya Sheria Ndogo, imebaini kuwa sheria nyingi zinazotungwa na mamlaka za serikali za mitaa zina kasoro, ikiwemo kukinzana na masharti ya Katiba.

Akiwasilisha ripoti ya kamati hiyo bungeni, jijini Dodoma, wiki iliyopita, mwenyekiti wake, Dkt. Jasson Rweikiza, alisema hali hiyo inasababisha matatizo makubwa kwenye utekelezaji wa sheria hizo ndogo na wakati mwingine utekelezaji wa Katiba.

Mwenyekiti huyo alisema utekelezaji wa sheria hizo unakumbana au kuzalisha matatizo mbalimbali, ikiwemo ugumu wa utekelezaji, matumizi mabaya ya madaraka na ukiukaji wa haki za kimsingi na uhuru unaohakikishwa na Katiba.

Dkt. Rweikiza alisema kipimo kikuu kili-chotumika kupima sheria hizo ni masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo lililoisaidia kamati yake kubaini sheria 38 zenye dosari.


Alizitaja dosari nyingine kuwa ni ukiukwaji wa uhuru wa raia na kudhoofika kwa utawala wa sheria, dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na

sheria mama au na sheria nyingine za nchi, kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za bunge, hivyo

kuvuruga mfumo wa sheria za nchi.

“Sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia, inasababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa masharti hayo...”

“Hali hiyo inaweza kuwa ni chanzo cha kukwamisha malengo ya sheria mama pia uwezekano wa mazalia ya kero kwa wananchi, dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na hata



Dkt. Jasson Rweikiza

kueleweka, hivyo, kuwepo kwa madhara wakati wa utekelezaji, jambo ambalo halikuwa lengo la bunge wakati wa kukasimu madaraka yake,” alisema Dkt. Rweikiza.

Aliongeza kuwa kuna dosari za uandishi wa majedwali katika sheria, jambo ambalo linaweza kusababisha sheria iliyoandikwa isieleweke ipasavyo kutokana na kukosekana kwa ufafanuzi uliokusudiwa.

Alibainisha pia kutokamilisha utekelezaji kwa baadhi ya maazimio ya bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo, kunachelewesha utatuzi wa kero za wananchi.

Msomi huyo alisema kasoro zilizopo kenye sheria ndogo zinaweza kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa.

“Hivyo basi bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi kama ilivyobainishwa katika taarifa, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo,” alisema.

Dkt. Rweikiza alisema dosari zinaweza pia kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo yenyewe na kuwa chanzo cha kero miongoni mwa wananchi.

Tiba ya Ukimwi yapatikana, lakini...

Na Mwandishi WETU

KATIKA mkutano mkubwa wa masuala ya Ukimwi uliofanyika Julai, mwaka huu, wanasayansi walitangaza kuwa mtu wa saba alikuwa amepona ugonjwa huo.

Huyo ni raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 60 ambaye naye alipona kupitia matibabu ya kupandikiza seli.

Mtu huyo amekuwa akiishi bila virusi vinavyosababisha Ukimwi kwa muda wa takribani miaka sita sasa, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na watafiti.

Huyu ni mtu wa kwanza anapona kwa kutumia matibabu hayo yaliyoanza mwaka 2008 katika hatua za utafiti kwa binadamu.

Hili linaweza kuwa jambo la kuleta furaha na faraja, lakini hali haipo hivyo kwa watafiti wenyewe na hata miongoni mwa wagonjwa.

Hii ni kwa sababu aina hii ya matibabu yanatumia teknolojia ya hali ya juu, hivyo kuyafanya kuwa aghali zaidi.

Nchi nyingi haziwezi kumudu gharama za matibabu haya, achilia mbali mgonjwa mmoja mmoja.

Watu wengi ambao wanasumbuliwa na ugonjwa huu wanatoka katika familia fukara, hivyo kutoziwezesha kumudu gharama za matibabu haya.

Hivyo, kugunduliwa kwa matibabu haya hakuleti faraja kwa sababu hakutawasaidia watu wengi duniani kulingana na hali ilivyo hivi sasa.

Pamoja na hayo, watalaamu wenyewe wame-shathibitisha kuwa matibabu haya yana hatari nyingi ikiwamo athari za maambukizi ya magonjwa mengine.

Wanasema ingawa kweli matibabu hayo yanaondoa virusi vya Ukimwi kutoka kwa aliyeambukizwa, lakini yanaleta uwezekano wa kuibuka kwa hatari nyingine nyingi na kubwa za kiafya kwa mtu huyo.

Watalaamu wanaeleza kuwa waliweza kufanya matibabu hayo kwa mtu huyu wa saba na alifanikiwa kupona Ukimwi kwa sababu yeye na mtu aliyetoa seli, wote walikuwa wanaugua saratani

ambayo matibabu yake yalihatiji kupandikizwa uboho, kwa mujibu wa Sharon Lewin, mtalaamu wa magonjwa ya kuambukizwa anayeongoza kituo cha Magonjwa na Kinga huko Melbourne, Australia.

Hivi sasa, matibabu yanayopendekezwa kwa mtu aliyeambukizwa Ukimwi ni matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV), yanayohusisha mseto wa dawa, ambazo aghalab, humezwa kila siku.

Dawa hizi huzuia vizuri vya Ukimwi kuongezeka mwilini mwa mtu aliyeambukizwa.

ARV kwa kawaida zinaweza kupunguza kiwango cha virusi kwenye mwili wa mtu aliyeambukizwa hadi kufikia hatua ya virusi hivyo kutoonekana kabisa, hivyo kupunguza uwezekano wa mtu huyo kumwambukiza mtu mwingine.

Lakini wengi wanaona kama ARV siyo matibabu mujarabu kwa sababu hayana uhakika.

Ndio maana watalaamu wamekuwa wakiendelea na kazi ya utafiti kuhusu tiba ya virusi hivyo.

Jitihada hizo za kutafuta tiba zinatokana na ukweli kuwa kuna usambazaji mdogo sana wa dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi hivi sasa, kuongezeka kwa usugu wa dawa hizo na unyanyapaa miongoni mwa walioambuikizwa virusi hivyo, mambo ambayo yanamaanisha kuwa watu wengi waliambukizwa VVU wanatamani kupatikana kwa tiba nzuri zaidi.



Dawa za ARV

Uchaguzi Marekani



Ikulu ya Marekani

Yanayowatenganisha wagombea urais

Na Mwandishi WETU

RAIA wa Marekani watamchagua kiongozi wa nchi yao Novemba 20, mwaka huu.

Wanaoingia kwenye kinyang'anyiro hicho ni wagombea wakubwa wawili ambao wanatoka vyama vikubwa vya Republican na Democrat.

Tayari vyama hivyo vimefanya uteuzi wa wagombea wao na sasa kivumbi kinahamia kwenye kampeni.

Republican kimemwamini Donald Trump, ambaye alipigwa mwereka na Joe Biden katika uchaguzi uliopita, Democrat kimeamua kwenda na Kamala Harris, makamu wa sasa wa rais.

Hii ni mara ya pili kwa chama cha Democrat kumteua mwanamke kuwa mgombea urais wake. Awali kiliwahi kumtea Hillary Clinton ambaye mwaka 2016 alishindwa mbele ya Trump.

Kwenye kampeni ndiko zinakoibuliwa hoja ambazo zinavitofautisha vyama hivi kuhusu sera zao kwenye mambo muhimu ambayo ita-

yasimamia iwapo mgombea wake atachaguliwa. Baadhi ya mambo hayo na misimamo ya vyama hivyo ni kama ifuatavyo;

Uchumi

Kwa muda wa miaka minne iliyopita, serikali ipo chini ya Rais Biden na baadhi ya watu wamebatiza jina la "Bidenomics" kama aina ya uchumi ambao kiongozi huyo wa Marekani amekuwa akiutekeleza.

Mfumo huo wa uchumi unajengwa chini ya msingi wa kujenga uchumi kutoka ngazi za chini. Hii inamaanisha kuwekeza kwenye miundombinu na sekta ya uzalishaji, matumizi ya nishati safi na kuongea nafasi za ajira.

Takwimu zinaonyesha kuwa mfumo huu umefanikiwa kwa kiasi fulani kwani uchumi unakua huku nafasi za ajira zikiongezeka.

Hata hivyo, wapiga kura wengi hawajaridhika na kupanda kwa mfumko wa bei, hasa za vyakula na petroli.

Inaendelea Uk. 17

Uchaguzi Marekani



Yanayowatenganisha wagombea urais

Inatoka Uk. 16

Trump naye amerusha lawama kwa Biden na serikali yake kwa kupandisha mfumko wa bei na ameahidi kuwa iwapo atachaguliwa, basi atachukua hatua za kushusha bei za bidhaa na huduma kwa kupunguza kodi.

Pia Trump ameshatangaza kuwa akishinda urais atamfukuza kazi mwenyekiti wa Benki Kuu, Jerome Powell, mtu ambaye yeye ndiye aliyemteua kushika nafasi hiyo, lakini sasa anamlaumu kwa kwa “mwanasiasa” zaidi.

Uhamiaji

Kuhusu uhamiaji, Democrat chini ya Biden kinafuata misingi ya kiotu, hasa kushughulikia wahamiaji kutoka Mexico na nchi nyingine zinazopakana na Marekani.

Ndio maana katika kipindi cha miaka minne iliyopita, serikali ya Democrat imefuta sera nyingi zilizotungwa na serikali ya Trump kuhusu masuala ya uhamiaji.

Lakini kuongezeka kwa idadi ya wahamiaji haramu kumeilazimisha Serikali ya Democrat kubadili msimamo wake na kubadili baadhi ya sera zake.

Iwapo kitashinda uchaguzi, rais ajaye wa Democrat anatarajiwa kutoa amri ambayo itawapa mamlaka maofisa kwenye vituo vya mipakani, kudhibiti idadi ya wahamiaji na pia kuwarejesha makwao watakaobainika kuingia nchini humo bila kufuata taratibu za kisheria.

Kwa upande wake, Trump anasema kuwa iwapo atachaguliwa, atafanya marejeio ya sheria na kuweka sheria kali ambazo zitafunga kabisa mipaka ya nchi hiyo kwa wahamiaji haramu.

Kama hiyo haitoshi, Trump ameshasema kuwa ataanzisha operesheni kubwa ya kihistoria kuwabaini na kuwarejesha makwao wale wote ambao wameingia nchini humo kinyume cha sheria.

Republican pia kimeahidi kisitisha utaratibu wa kuwapatia uraia watoto waliozaliwa nchini humo na wahamiaji haramu.

Utoaji mimba

Democrat kinamlaumu Trump kwa sera zake kali zinazopinga uhuru wa kupanga uzazi.

Hii ni baada ya mahakama ya juu chini ya majaji watatu walioteuliwa na Trump kubatilisha hukumu ya mwaka 1973 iliyowapa uhuru wanawake nchini humo haki ya kikatiba ya kutoa mimba.

Democrat kimeshasema kuwa iwapo kitashinda kitarejesha haki hiyo.


Lakini moja kati ya mambo ambayo Trump anajivunia ni kuondoa haki hiyo.

Lakini anaonekana kulainisha msimamo wake akisema kuwa akishinda, atayaruhusu majimbo kuwa na haki ya kujitungia sheria kuhusu masuala la utoaji mimba.


Misaada kwa Ukraine

Democrat chini ya Rais Biden kimelishauri Baraza la Congress kuendelea kufadhili Ukraine, kikionya kuwa ushindi wa Urusi dhidi ya Ukraine, kutaiweka Ulaya hatarini na kumpa nguvu adui mwingine mkubwa wa Marekani, China.

Inaendelea Uk. 18



Kamala Harris



Uchaguzi Marekani

Yanayowatenganisha wagombea urais

Inatoka Uk. 17

Lakini Trump ameshaonya kuwa ataiacha Urusi ifanye inavyotaka kwa nchi wanachama wa NATO iwapo nchi hizo hazitatoa mchango wao stahiki wa kifedha.

Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni, anaonekana kulainisha msimamo huo.

Vita vya Israel vs Gaza

Serikali ya Biden imekuwa ikitoa mabilioni ya dola na vifaa vya kivita kama msaada kwa Israel na kuhimiza misaada zaidi kwa nchi hiyo.

Lakini hivi sasa inakabiliwa na lawama kutoka kwa wananchi ambao hawafurahishwi na jinsi Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu anavyoshughulikia suala na vita huko Gaza.

Akiwa muungaji mkono mkubwa wa Israel, Trump ameahidi kuwa akishinda "atamalizia kile ambacho alikianza" dhidi ya wanamgambo wa Hamas huko Gaza.

Kodi

Serikali ya Democrat imetangaza kuongeza kodi kwa mashirika hadi asilimia 28.

Hiki ni kiwango kinachokaribia asilimia 35 ambacho kiliwekwa wakati wa utawala wa Trump.

Democrat pia kimeshaeleza azma yake ya kuwa na kodi kubwa kwa matajiri, kuwa na mikakati ya kukabiliana na ukwepaji kodi, na kutoa nafuu ya kodi kwa watu maskini.

Hivi karibuni Rais Biden aliongeza ushuru kwa bidhaa kutoka China, ikiwamo ongezeko la asilimia 100 kwa ushuru wa magari ya umeme.

Kwa upande wake, Trump ameahidi kupunguza kodi katika matabaka yote kwa kuanzia na kuhiisha punguzo la kodi ya mapato linalokaribia kufikia mwisho wake.

Pia ameahidi kutoa nafuu kwa kodi kwa matajiri hasa kupitia sheria aliyoisaini mwaka 2017.

Anasema ataacha kodi ya mashirika kwenye kiwango cha asilimia 21 na anapendekeza kiasi cha asilimia kumi cha ushuru wa bidhaa zinazozingizwa nchini humo na ushuru wa asilimia 60 kwa bidha zitakazozingizwa kutoka China.

Afya

Democrat kinapendekeza kushushwa kwa gharama za matibabu na dawa kwa wazee.

Wakati bima ya afya maarufu kama "Obamacare" ikiendelea kupata umaarufu, chama hicho kimeendeela kuja na mipango ya kupanua wigo wa wanaonufaika na bima hiyo, jambo ambalo limewavutia watu wengi.

Lakini mara nyingi Trump amesema kuwa iwapo atashinda ataifuta bima hiyo na kuanzisha bima nyingine nafuu zaidi, lakini kila anapoulizwa anashindwa kutoa ufafanuzi wa anachokusudia kukifanya.

Kila mara amekuwa akitanusha tuhuma kuwa yeye na chama chake wanapanga kufuta mipango ya huduma za kijamii kwa familia masikini.

Uhalifu

Democrat chini ya Biden kimekuwa kikithamini sana uwekezaji kwenye suala la usalama wa raia na hivyo kusababisha kushuka kwa uhalifu ingawa kwa kiasi kidogo.


Takwimu za hivi karibuni kutoka FBI zinaonyesha kuwa uhalifu unashuka, ingawa wananchi wengi bado wanaona uhalifu unaongezeka.

Hivi karibuni mamlaka jijini New York zilizilazimika kuwatumia walinzi kufanya doria njia za treni chini ya ardhi kutokana na kuongezeka kwa uhalifu.

Wakati huohuo, Trump amekuwa akiwalaumu wahamiaji haramu kwa kuongeza uhalifu nchini humo.

Mara nyingi anatolea mfano wa ongezeko la uhalifu katika majiji yanayoongozwa na Democrat, akishutumu kuwa chama hicho kinakumbatia uhalifu.

Ameshapendekeza kuwa adhabu ya kifo iliyowekwa kwa watu wanaokutwa na hatia ya makosa ya kubeba, kutunza, kusafirisha na hata kuuza dawa za kulevya.



Donald Trump

Waziri wa Afya sikiliza kilio chetu madaktari, tusaide

Kwako Waziri wa Afya,

SISI ni wamiliki wa hospitali binafsi nchini Tanzania, ambao tumekuwa tukitoa huduma za afya, ikiwamo kushauri na kutibu changamoto za kiafya kwa Watanzania wenzetu.

Hakika mchango wetu ni mkubwa kwani na wenye umuhimu kwa kila mmoja.

Tunaleta barua maalum kwako kupitia gazeti hili la Pambazuko, kwa kuwa ndiyo tunaona ni njia sahihi na yenye kukufikia kwa haraka moja kwa moja, tukiwa na imani kwamba utaweza kusaidia kutatua malalamiko yetu.

Sisi tunaomba kuruhusiwa kuanza kupata vibali vya kusajili vituo vya afya vinavyotoa huduma za kibingwa (Polyclinics) na pia kuingizwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

Kama utakumbuka, serikali iliweka zuio la kusajili vituo hivyo vya kutolea huduma kwa wananchi, hali ambayo imekuwa ikisababisha madhila mengi kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za haraka jirani na maeneo yao.

Sisi tunatambua kuwa hakuna vituo vipya vilivyosajiliwa katika Mfuko wa NHIF tangu Aprili 2022 bila kutoa taarifa rasmi ya kusitisha usajili wa vituo vipya vya kundi hilo.

Takwimu za Wizara ya Afya zinabainisha kwamba mpaka kufikia mwezi Machi 2022 kulikuwa na jumla ya Kliniki za Kibingwa 299 ambazo ni sawa na asilimia 3.3 tu ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya Tanzania, chini, hivyo inaonekana wazi kwamba bado kuna uhitaji wa huduma hizo, tena zikiwa zimesajiliwa na NHIF, ili kuokoa afya za wananchi.

Mbali na kukosekana kwa huduma za haraka za afya jirani na makazi ya watu, pia kusitishwa kwa usajili wa vituo hivyo vya kibingwa, kunawanyima ajira madaktari wapya ambao wametoka mafunzoni.

Hali hii pia, inakwamisha jitihada za serikali



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama

kupunguza idadi kubwa ya watu wasiokuwa na ajira, hata kama wamesoma na kuhitimu wakiwa na utaalamu muhimu zaidi, kama udaktari.

Sisi tunatambua kuwa zipo Kliniki za Kibingwa zaidi ya 150 zimekwama kusajiliwa na NHIF, licha ya vituo hivyo kukidhi vigezo vyote vilivyoainishwa na mfuko na kwamba baadhi yake vilishafanyiwa tathmini ya vigezo na kuonekana kuwa na sifa za kusajiliwa ili kuhudumia wanufaika wa mfuko huo, lakini kinyume na matarajio, mchakato huo ulisitishwa bila taarifa yeyote kutoka kwa mamlaka.

Kutokana na hatua hiyo, kumekuwa na changamoto za kupungua kwa upatikanaji wa huduma, kuathiri uwekezaji katika Sekta ya Afya na kupunguza ari ya wawekezaji, kukwaza ubunifu na uboreshaji wa huduma na kuongeza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za umma.

Tunapendekeza kwamba ugozi wa wizara pamoja na ule wa NHIF kufanya mapitio ya zuio kwa kuzingatia athari zake kwa sekta ya afya na kwa wananchi wanaotegemea huduma za kliniki hizi na kuruhusu kusajiliwa kwa vituo ili kuimarisha afya za Watanzania na pengine kuokoa uhai.

Ni sisi wamiliki wa hospitali binafsi.



Habari Kuu

Yaelekea kuwa mazoea kuteka, kuua



Sheikh Ponda Issa Ponda

Inatoka Uk. 8

Askofu Munga

Askofu (mstaafu) wa Kanisa la Kiinjili la Kिलutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Dkt. Steven Munga, amesema jambo la kushangaza na kusikitisha ni kusikia kwamba watu wanapotea, lakini hakuna maelezo yeyote kutoka vyombo vyenye wajibu wa kuhakikisha usalama wao.

Dkt. Munga amesema wakati makundi mbalimbali katika jamii yana wajibu tofauti, lakini kuna vyombo vya serikali vyenye wajibu mkubwa zaidi, kama vile vyombo vya ulinzi na usalama, ambavyo vinapaswa kuzuia mapema

mambo haya.

“Hawa wahusika wasipowajibika ipasavyo, hufanya hata juhudi za wengine kufifia. Ukimya kwa vyombo vya ulinzi na usalama na ukimya kwa taasisi zinazotegemewa ziseme neno, ni dalili kwamba jamii imetiwa ganzi.”

“Lakini pia inaelekea ganzi ile ilitoa mwan-ya wa kuibuka vyombo bandia vinavyojitwalia mamlaka ya kuteka na kutesa wale wote wanaoonekana wako kinyume na matakwa yao.”

“Ukiukwaji wa kiwango cha juu kwa haki za watu katika awamu iliyopita, kumepandikiza hofu ya kupitiliza katika mioyo ya watu. Hofu ile inaelekea kukomaa kuwa ulemavu wa kudu-mu kwa jamii yetu,” ameingiza Askofu Munga.

Orodha ya TLS waliotekwa

Agosti 9 mwaka huu, TLS ilitoa tamko kuhusu ongezeko la matukio ya kutekwa, kupotea, na kuteswa kwa watu nchini Tanzania, na kudai kuwa vyombo vya dola vimeshindwa kutoa ufa-fanuzi wa kuridhisha au kuchukua hatua stahiki dhidi ya vitendo hivyo vya kikatili.

Kupitia kwa kiongozi wake, Wakili Boniface Mwabukusi, TLS kilitoa orodha ya watu 83 ambao tayari wamepotea au kutekwa kwa njia za kutatanisha kuanzia mwaka 2016 hadi 2024.

Aidha, chama hicho kilipendekeza kuanzish-wa kwa chombo maalum cha kudumu kitaka-chokuwa na jukumu la kusimamia na kuangalia utendaji wa vyombo vya dola, hasa Jeshi la Polisi.


Sheikh Ponda

Katibu Mkuu wa Taasisi ya Shura ya Maimam Tanzania, Sheikh Ponda Issa Ponda, ameliambia Pambazuko kuwa inasikitisha kuona Watanza-nia hawapigi kelele za kutosha kulaani vitendo vya utekaji, utesaji na watu kupotea, ambavyo kimsingi vilianza kwenye utawala wa awamu ya tano.

Inaendelea Uk. 21



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Yaelekea kuwa mazoea kuteka, kuua

Inatoka Uk. 20

Amesema kuendelea kwa matukio hayo bila hatua madhubuti kuchukuliwa, ni ishara kwamba usalama wa raia upo shakani.

“Serikali ina wajibu wa kulinda uhai wa watu, lakini ukishaona watekaji wana vifaa vya kuteka watu, yakiwamo magari na silaha na havipati upinzani wowote ujue usalama wa raia upo shakani,” amesisitiza.

Mwaka 2023 Sheikh Ponda kupitia taasisi yake, walifanya utafiti na kubaini familia 200 zilipotelewa na ndugu, jamaa, marafiki na watu wao wa karibu Tanzania Bara na Zanzibar.

Sheikh Ponda alisema wakati wakizindua ripoti hiyo walizialika taasisi za vyombo vya dola na haki za binadamu lakini wawakilishi wa vyombo vya dola hawakuhudhuria.

Askofu Bagonza

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania – Karagwe, Dkt. Benson Bagonza, akizungumzia kutekwa na kifo cha Ali Mohammed



Askofu Dkt. Steven Munga

Kibao, amesema ameshtushwa na kujawa taaruki baada ya kusikia kuuawa kwa kada huyo wa Chadema.

Anasema katika mazingira ya sasa, inawezekana kusema ni kosa na kwamba hata ukikaa kimya, inawezekana kuwa kosa linaloweza kuwakera watekaji.

Anasema kuna kila dalili kwamba kiongozi yeyote akijitokeza kusema ataitwa mchochezi na mvurugaji wa amani. Lakini kiongozi akikaa kimya atakuwa anaunga mkono wanaoteka na kuua, hivyo anaasa watu kuchagua kwa busara.

Dkt. Bagonza anasema kuna tafsiri moja kuu inayowahusu wanaoteka na kuua. Kama ni serikali au sehemu yake, watekaji na wauaji hawa hawana imani na utawala wa sheria na mahakama zetu.

Anasema kama wauaji ni watu binafsi, basi nao wanaoudharau sana mfumo wetu wa utawala wa sheria.

Anaendelea kueleza kuwa watekaji wa Kibao walikuwa na pingu, bunduki, magari maalum na walizuia barabara. Vitu hivi ni hatari kuwa katika miliki ya raia bila utaratibu.

Dkt Bagonza anahoji, watu waliomteka Kibao kujitambulisha kuwa ni polisi na kueleza kama ni polisi, basi watakuwa wamewatukana Watanzania wote na kuwa kama siyo polisi, basi wamelitukana Jeshi la Polisi.

Akizungumzia kutekwa na kupotezwa kwa kada wa Chadema, Deusdedit Soka, anasema huenda Soka ametekwa na wajanja wanaotumia jina la polisi (Rogues); na kutokamatwa kwao ni hatari kwa kila mtu na kila taasisi; hivyo wakiishazoea watateka viongozi wetu na kusababisha hali ya hatari.

Watekaji wasiokamatika ni sawa na silaha moja kupotea kutoka ghala la silaha na anaongeza kuwa Jeshi la Polisi liko lawamani katiika nadharia hii.


Kauli ya Jeshi la Polisi

Baada ya kupokea taarifa za kutekwa na kuuawa kwa Kibao, ambaye ni kiongozi wa Chadema jana, Jeshi la Polisi lilitoa taarifa kwa umma na kueleza kuwa linafanya kila linaloweza kuhakikisha linapata nini kilitokea na pengine wahusika wa mauaji hayo ya kikatili.



Kenya

Ruto vs Kalonzo uchaguzi mkuu 2027



Kalonzo Musyoka



Rais wa Kenya, William Ruto

Na Juloius MKAMBI, Nairobi

KENYA ni kama iko tofauti. Inakwenda haraka mno kulinganisha na nchi zingine za Afrika Mashariki. Ona sasa, wanasiasa wake wameanza kujipanga kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2027.

Hali hiyo imethibitika wivi karibuni, wakati wa ziara ya Rais William Ruto eneo la Nyanza. Eneo hilo ni ngome kuu kisiasa ya kiongozi wa upinzani, Raila Odinga.

Rais Ruto akiwa Kisumu alipokewa na umati mkubwa tofauti na ilivyokuwa kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2022, ambapo msafara wake ulishambuliwa kwa mawe kutokana na upinzani wa kisiasa kati yake na Raila wakati huo wote wakiwania urais.

Utulivu huo huenda umetokana na ukaribu wa Ruto na Raila kwa siku za hivi karibuni na upepo wa siasa nchini Kenya umebadilika mno, ikizingatiwa awali ilionekana uswahiba wao ni wa 'nipe nikupe.'

Rais Ruto baada ya kutambua kuwa hawezi kufanya kazi ya "kutuliza" Wakenya bila Raila,

akaamua kufanya naye kazi.

Ukaribu wa viongozi hawa wawili ulishuhudia Rais Ruto akiteua viongozi wanne waandamizi wa Chama cha Orange Democratic Movement (ODM) kushika nyadhifa za uwaziri.

Akiwa ziarani Kisumu katika ngome ya Raila, Ruto alidokeza mpango wa chama chake cha United Democratic Alliance (UDA) kuungana na ODM katika uchaguzi mkuu ujao.

Hali ilivyosasa haijulikani kama ODM ipo upinzani au serikalini, licha ya Naibu Kiongozi wa ODM ambaye pia ni Gavana wa Mombasa, Abdulswamad Shariff Nassir, kusisitiza chama hicho kinabaki imara ndani ya Azimio la Umoja ambayo ni muungano wa vyama vya upinzani.

Ni dhahiri Rais Ruto atawania tena muhula wa pili kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2027, ila maswali ya kujiuliza ni je, atatumia chama gani? Ataungana na wanasiasa gani wenye majina makubwa na ushawishi Kenya?

Mgombea ambaye anatajwa angekuwa tishio kwa Ruto kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2027, bado alibaki kuwa Raila, lakini sasa kiongozi huyo wa ODM ameanza kuwasongesha wanachama wake kumuunga mkono Rais Ruto.


Aidha, kuna nafasi finyu ya Raila kuwepo "debeni" 2027 kwa sababu akifanikiwa kuchaguliwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AUC), atahudumu kwenye wadhifa wake mpya kwa muda wa miaka minne, ambapo katika kipindi hicho, Kenya itakuwa inakwenda kwenye uchaguzi mkuu.

Hivyo, aliyejitokeza wazi, siyo tu kuvaa via-tu vya Raila akiwa kiongozi wa upinzani, bali hata kutangaza kuwania urais 2027, ni Kalonzo Musyoka.

Kalonzo ambaye ni kiongozi wa Chama cha Wiper, aliwahi kuwa makamu rais chini ya utawala wa Mwai Kibaki, na ni moja wa viongozi waandamizi ndani ya Azimio la Umoja.

Waliosalia kwenye upinzani wanamtaka Kalonzo kuanza kuzunguka nchi nzima kuimari-sha upinzani ikiwemo pia kujipanga katika safari yake ya kumgoa Rais Ruto uongozini kupitia njia ya demokrasia.

Je wajua



Kwale ni ndege wadogo, wenye urefu wa sentimita 18 hivi na uzito upatao gramu 100. Wanazaana katika maeneo mengi ya Asia magharibi na Ulaya. Kwa kuwa kware ni ndege wa kuhamahama, wao huhamia Afrika Kaskazini na Arabia wakati wa baridi kali.



Tabasamu 'huambukiza' mtu anapotabasamu huweza kumfanya mtu mwingine naye kutabasamu, sababu tunapenda kufanya hivyo ili kupata hisia sawa kama anayopata mtu anayetabasamu.

China kukopesha tril. 138/-...

Inatoka Uk. 4

“Na ni chini ya asilimia 12 ya thamani halisi ya madini hayo ambayo imekuja katika nchi hizi za Afrika, kwa hiyo utaona kwamba ipo changamoto kubwa inapokuja kwenye rasilimali zenyewe..”

“Bila shaka, kwa suala la Tazara Pamoja na kwamba zitakuwepo shughuli ndogondogo zinazofanyika, bado mzani utakuwa umelalia sana kwa upande wa China,” amesema Dkt. Kahyoza.

Amesema katika mkutano huo, viongozi wa Afrika walikuwa na masuala kama matatu makubwa, kwanza ni suala la miundombinu, ili kuendelea kuimarisha miundombinu kama ya reli na barabara.

Pia agenda ya kuimarisha sekta ikiwemo ya kilimo na kuhuisha uchumi wa Afrika kuwa kwenye maeneo muhimu ya kidigitali.

“Bila shaka ni agenda ambazo kinadharia unaona kwamba zinauzika kwa kiwango kikubwa ila kwa upande wa pili agenda hizi zinakuwa hazijazama sana kwenye masuala na maslahi mapana ya bara lenyewe,” ameingiza Dkt. Kahyoza.

Ameeleza kuwa ukiangalia, pamoja na jitihada hizi za kuwekeza kwenye miundombinu, imekuwa haiziongezei kwa kiwango kikubwa manufaa ya kibiashara.

Kwamba ukiangalia nakisi ya kibiashara kati ya Afrika na China hivi leo, ni takribani dola bilioni 64 kwa takwimu za mwaka 2023.

Msomi huyo amesema kiasi hicho ni zaidi ya fedha ambazo China iliipa Afrika kwenye mkutano kama huu mwaka 2018,

yaani ni zaidi ya asilimia 40 ya fedha yote ambayo Afrika imeliipa kuhudumia deni lake ambalo limetoka karibu dola bilioni 60 mwaka 2010 hadi kufikia dola bilioni 165 mwaka 2023.

Dkt. Nguma

Mtaalamu na mchambuzi wa masuala ya Uchumi, Dkt. Walter Nguma, ameliambia Pambazuko kuwa mkutano huo ni ishara kuwa diplomasia kati ya mataifa ya Afrika na yale ya Ulaya na Asia, hususani China, yanazidi kuimarika kwa kasi kutokana na ushindani uliopo duniani.

“Hii ndiyo maana nchi hizi zinaona kuwa namna pakee ya kuweza kuishika Afrika ni kutoa misaada kulingana na uhitaji wa kifedha kwa nchi za bara hilo na ndiyo jambo linaloonekana haraka kwamba hiyo mikopo ni ya kutafuta kuona namna gani wanaweza kupata eneo kubwa ili kujivunia ukumbwa wao,” ameingiza.

Kuhusu Tazara

Dkt. Nguma amesema makubaliano ya uboreshaji wa Reli ya Tazara ni muhimu kwa sasa kwa sababu ina historia ndefu tangu kujengwa kwake.

Ameeleza kuwa reli hii iko kwenye mioyo ya watu na ya viongozi wa China, kwa sababu ilitakiwa ijengwe na mataifa mengine, lakini yalivyopima yakaona haina maslahi makubwa kwao kiuchumi.

Daktari huyo wa uchumi amesema kwa China ilikuwa na migogoro na nchi mbalimbali na iliamua kujenga rdei hiyo kama sehemu ya kujiimarisha kimataifa.



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Nabii Mwingira atulize upepo mchafu unaovuma



Nabii, Josephat Mwingira

HIVI karibuni Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo, alionyesha masikitiko yake makubwa kuhusu unyanyasaji na ukiukwaji wa haki za binadamu unavyofanywa na walinzi wa shamba linalomilikiwa na Kanisa la Efata, lililo chini ya Mtume na Nabii, Josephat Mwingira.

Katika maelezo yake bungeni, Shigongo ambaye alisema wazi kwamba ni mlokole, aliongea kwa hisia kali akionyesha kuguswa na kutofurahishwa kabisa na ukiukwaji huo wa haki za binadamu unaofanywa na walinzi waliowekwa kwenye shamba la kanisa.

Pamoja na hayo, Shigongo aliuliza wabunge endapo Mtume na Nabii Mwingira ni mtumishi wa Mungu kwa sababu maovu yanayofanyika katika shamba hilo lililoko Malonje, Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, hayaendani na sifa za kiroho alizonazo kiongozi huyo wa dini.

Sitaki kuhoji kama Mwingira ni mtumishi wa Mungu kwa sababu nikifanya hivyo nitakuwa simtendei haki kiongozi huyo wa dini, ingawa taarifa za mgogoro wa shamba hilo nimekuwa nikizisikia kwa miaka mingi.

Naamini Mwingira alimsikia Shigongo alipokuwa akishusha lawama dhidi yake, na pia alisikia jinsi Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson, alivyoingilia kati mchango wa mbunge huyo ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari na naamini pia habari ya kuhusishwa kwake na ukiukwaji wa binadamu, ilijadiliwa na baadhi ya waumini wa makanisa yote anayoyasimamia hapa nchini.

Naamini pia Mwingira ameipata na kuisoma ripoti ya Kamati Maalum ya Bunge iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni kuhusiana na shamba hilo la Malonje.

Naamini katika kusoma huko, Mwingira ameelewa kile kilichoandikwa kwenye ripoti hiyo.

Sijui atakuwa amejisikiaje kwa kanisa lake kuhusishwa na madhila kwa binadamu, lakini sisi wengine ripoti ya kamati hiyo imetusikitisha sana, hasa ukizingatia kuwa ukiukwaji wa haki za binadamu unaotajwa, umefanywa na watu ambao tunadhani ndio wanapaswa kutuongoza kwa kuwa na huruma kwa binadamu wengine.

Sasa basi, kilichobaki ni kiongozi huyo wa dini kujitokeza hadharani na kueleza umma juu ya tuhuma hizo dhidi ya taasisi inayoiongoza.

Labda, kwa kuwa habari hizo zimeongelewa na upande mmoja, kuna mambo ambayo yapo upande wake ambayo umma unapaswa kuyasikia pia.

Mwingira asikae kimya na kuziba masikio akijifanya hajasikia kilichotokea bungeni. Asitumie muda mwingi kuhubiri injili wakati kanisa lake linahusishwa na mambo yanayomchukiza Mungu, bali ajitokeze kwa mazingira atakayoona yanafaa ili kusafisha upepo mchafu unaomzonga kila anapokwenda.

Anaweza kutumia vyombo vyake vya habari na hata vingine kueleza umma anachokifahamu kuhusu shamba hilo, ambalo sasa linahusishwa na tuhuma ambazo haziendani ya mafundisho ya Mwenyezi Mungu yanayotueleza kuwa na matendo ya huruma, kutoonea wala kutesa viumbe wa Mungu aliowaumba kwa mfano wake.



Ngorongoro bado wamtaka Samia

Na Maregesi PAUL

WAKATI hatua mbalimbali zikiendelea kuchukuliwa na serikali kutekeleza ahadi kwa wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro, bado wanasisitiza wanahitaji kukutana uso kwa uso na Rais Samia Suluhu Hassan.

Wakizungumza na Pambazuko jana wamesema kuwa wanashukuru kuwa hadi sasa serikali imeonyesha nia ya kutekeleza ahadi zilizotolewa kurejesha huduma za jamii katika eneo hilo, lakini ili wawe na uhakika zaidi wangependa kukutana na kiongozi mkuu wa nchi.

Wiki iliyopita washauri wawili wa Rais Samia, Abdallah Bulembo na Balozi Rajab Luhwavi, walikuwa katika tarafa hiyo wakikagua na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na kiongozi wa nchi kupitia kwa viongozi kadhaa serikalini.

Pambazuko limeelezwa kuwa kikao cha ndani cha washauri hao wa Rais Samia na viongozi wa kimila wa eneo hilo kilifanyika Oktoba 5, mwaka huu, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ngorongoro iliyoko katika Kata ya Alaitole.

Kwa mujibu wa chanzo hicho, kikao hicho kilianza siku hiyo saa saba mchana, kikiongozwa na Diwani wa Alaitole, James Moringe na kilimalizika saa 12:30 jioni baada ya kuhudhuriwa na washiriki wapatao 140 kutoka katika kata saba za Kakesyo, Alaitole, Enduleni, Misigiyo, Albalbalu, Ngoile na wengine walitoka katika Kata ya Eyasi.

Chanzo chetu hicho kilidokeza zaidi kuwa washiriki kutoka katika kata nne za Lainolkanolka, Naiyobi, Alailelai na Ngorongoro, hawakushiriki kwa kile kilichoelezwa kuwa walikosa usafiri wa kuwafikisha maeneo ya mkutano.

Aidha, chanzo hicho kilifafanua kwamba, kikao hicho kilifanyika kwa utulivu wa hali ya juu, ila baadhi ya washiriki walieleza wazi wazi jinsi walivyokerwa na kitendo cha kuondoa huduma za jamii katika kata zao na kueleza jinsi walivyokuwa wamejipanga kuwafungulia mashata baadhi ya viongozi wa serikali.

Wakazi wa Ngorongoro, wengi wakiwa wafu-

gaji wa Kabila la Wamasai, walisisitiza kuwa hata kama viongozi wengi wa serikali watatembelea makazi yao kwa ajili ya kutatua kero zao, hawawezi kuwaamini hadi Rais Samia mwenyewe atakapofika Ngorongoro na kuzungumza nao.

Wafugaji hao wameweka msimamo huo pia mwishoni mwa wiki, walipokuwa wakizungumza katika kikao cha viongozi wa kimila kilichohudhuriwa na washauri wawili hao wawili wa Rais Samia.

Bulembo na Balozi Luhwavi, walikuwa Ngorongoro wiki iliyopita kwa ajili ya kutembelea tarafa hiyo na kuona hatua zinazoendelea kutekeleza ahadi za Rais Samia kwa wakazi wa eneo hilo.

Rais Samia aliahidi kurejesha huduma za kijamii kwa wakazi hao, baada ya kusitishwa kwa muda kufuatia zoezi la kuwahamisha na kuwapeleka Msomera, Handeni, mkoani Tanga.

Hatua ya kuhamisha wakazi hao ilizua sokomoko, baada ya wengi kugomea mpango huo wa serikali, hivyo iliamua kusitisha huduma za kijamii, ikiwa ni njia ya kuwashinikiza kuhama.

Rais Samia pia aliagiza kurejesha kwa haki ya wakazi hao kupiga kura katika eneo lao, baada ya kuwa majina yao yamehamishiwa vituo vya kupigakura Msomera.

Agosti, mwaka huu, viongozi waandamizi wa serikali; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), William Lukuvi alikuwa Ngorongoro akiambatana na Waziri wa Kati ba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi kwa ajili ya kuwasilisha ahadi ya Rais Samia.

Rais Samia alitoa agizo hilo baada ya maelfu ya wafugaji hao kuandamana kwa amani kwa siku tano mfululizo hivi karibuni, wakipinga kusitishwa kwa huduma za jamii katika eneo lao kama sehemu ya kuwalazimisha wahamie katika Kijiji cha Msomera.

Awali ilielezwa kwua uhamaji huo ni wa hiari, lakini serikali ikasitisha huduma nyingi za kijamii ikiwamo haki ya watu hao kupiga kura baada ya kuhamisha majina ya wapiga kura wote huko Msomera.



Makala

Mpox inaambukiza kwa ngono, chukua tahadhari



Na Hellen NGOROMERA

DUNIA inahangaika sasa kutokana na kuibuka kwa tishio la homa ya nyani au kwa kifupi Mpox.

Huu ni ugonjwa unaoambukiza binadamu, lakini ukisababishwa na virusi ambavyo asili yake ni nyani vinavyojulikanaavyo kama monkeypox.

Hivi karibuni, virusi vya ugonjwa huo viligunduliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kabla havijasambaa katika nchi jirani za Kenya, Rwanda na Uganda.

Taarifa zilizotolewa mapema mwezi huu, zinaeleza kuwa tayari maambukizi ya homa hiyo yamegundulika katika moja ya nchi za Ulaya.

Hata hivyo, Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, amewahakikishia Watanzania kuwa bado ugonjwa huo haujaingia nchini.

Anasema tayari wizara imechukua hatua za kuilinda nchi dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Aidha, amebainisha kuwa maandalizi kabambe yameshafanyika kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa haraka iwapo utaibuka nchini.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, kati ya hatua zilizochukuliwa kulinda nchi na watu wake, ni pamoja na kuimarisha uchunguzi kwa wasafiri kupitia huduma za afya mipakani ikiwemo bandari, nchi kavu na viwanja vya ndege ili kuwabaini wasafiri wenye viashiria na dalili za ugonjwa huo.

Waziri Mhagama anasema wizara, kwa kushirikiana na wataalamu wa afya, imejipanga kufuatilia na kuhakikisha kuwa mtu atakayeambukizwa, anapata

huduma muhimu kwa haraka ili kuepuka kuenea kwa virusi hivyo.

WHO yalonga

Taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinasema kuwa ugonjwa huo umeendelea kuenea katika nchi mbalimbali duniani na kwa takwimu za kipindi cha Januari 2022, hadi 30 Juni 2024, jumla ya wagonjwa 99,176 wamethibitika kuambukizwa Mpox katika nchi 116 duniani kote na kati yao na watu 208 sawa na asilimia 0.2 walipoteza maisha.

WHO inaeleza kuwa kati ya maambukizi yote yaliyoripotiwa, Bara la Afrika limethibitisha maambukizi 4,232 sawa na asilimia 4.3 ya wagonjwa wote duniani.

Mabara yanayoongoza kuwa na maambukizi mengi ni Amerika ya Kaskazini na Kusini yakiwa na maambukizi 62,904 sawa na asilimia 63.4 yakifuatiwa na Bara la Ulaya lenye maambukizi 27,529, sawa na asilimia 27.8 ya maambukizi yote duniani.

Kutokana na hali hii, Waziri Mhagama ametoa rai kwa jamii kutoa taarifa za watu wenye viashiria au dalili za ugonjwa huo kwa kupiga simu bure kwenda namba 199 kwa ajili ya kupata huduma.

Mhagama anawasihi watu watakaokuwa karibu na mtu anayehisiwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo, kuepuka kugusana kwa njia ya kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana, kujamiiiana na mtu mwenye dalili za Mpox au kugusa majimaji kutoka katika mwili wa mgonjwa.

Hatua nyingine ambazo mtu anapaswa kuzichukua ili kukabiliana na maambukizi ya Mpox, ni pamoja na kunawa mikono kila mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.

Mhagama ametoa mwito kwa maeneo ya umma, kaya na taasisi mbalimbali, ikiwemo shule, vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya, kuhakikisha kunakuwa na vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni.

Alizitaka familia ambazo atatoka mtu anayehisiwa au aliyeambukizwa ugonjwa huo, kuhakikisha wanasafisha na kutakasa vyombo vilivyotumika na mgonjwa huo.

Usafi wa vifaa hivyo unaweza kufanyika kwa kutumia sabuni au klorini (mfano Jik) na kuepuka kula au kugusa mizoga au wanyama ambao wanaweza kuwa na maambukizi.



Mpox inaambukiza...

Inatoka Uk. 26

Kama ilivyokuwa wakati wa Covid-19, Mhagama amewakumbusha Watanzania kuanza kuvaa barakoa kwa tahadhari iwapo itabidi kukaa na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za Mpox.

Dalili

Dalili kubwa ya ugonjwa huu ni homa, maumivu ya kichwa, uvimbe, maumivu ya mgongo na misuli kuuma.

Mara baada ya kupata homa, upele unaweza kutokea, mara nyingi huanza kwenye uso kisha kuenea kwenye sehemu nyingine za mwili, viganja vya mikononi na nyayo za miguu.

Upele unaweza kuwasha au kuuma, na hubadilika hatua tofauti kabla kutengeneza malengenge ambayo hupasuka na kusababisha vidonda na hatimaye makovu.

Maambukizi kwa kawaida huisha yenyewe na hudumu kwa kati ya siku 14 na 21. Lakini kuwa wakati hali inakuwa mbaya kiasi kuwa malengenge yanayopasuka husababisha vidonda kwenye maeneo mengi ya mwili ikiwemo mdomo, macho na sehemu za siri. WHO inashauri ikiwa mtu umeambukizwa Mpox, unapaswa kujitenga kwa kipindi chote cha maambukizi hadi upele utakapopasuka. Pia kufunika vidonda na kuvaa barakoa kunaweza kusaidia kuzuia kuenea.

Mambo ya kufanya

Profesa wa afya ya binadamu kutoka Taasisi ya London School of Hygiene & Tropical Medicine (LSHTM), Michael Marks, amenukuliwa na Shirika la Utangazaji la BBC akisisitiza jumuiya ya kimataifa kuyachukulia maambukizi haya kwa umakini mkubwa kwa sababu yanaweza kugeuka kuwa 'maambukizi ya kimataifa.'

Amesisitiza kuna uwezekano wa kuudhibiti ugonjwa huo kirahisi katika siku hizi za mwanzo za mlipuko, lakini ukiachwa usambae itakuwa vigumu kuudhibiti baadaye.

Ameitaka jumuiya ya kimataifa kusaidia nchi kama vile DRC na nyinginezo zenye maambukizi hivi sasa ili kuutokomeza ugonjwa huo.

Unavyosambaa

Njia kuu ya kuenea kwa maambukizi ni kugusana

moja kwa moja kimwili na vidonda kwenye ngozi ya aliyeambukizwa.

Pia ugonjwa huu unaambukiza kwa njia ya ngono, lakini pia inaweza kutokea kwa kugusana kawaida, kwa mfano kugusana na mtoto wako.

Profesa Marks anasema kufanya ngono kuna chukua sehemu kubwa ya maambukizi ya janga hilo la Mpox.

Chanjo

Profesa huyo anasema jambo kubwa litakalosaidia kupambana na maambukizi haya ni upatikanaji wa chanjo.

Lakini hivi sasa nchi nyingi zenye maambukizi, hasa barani Afrika, hazijapata chanjo ya ugonjwa huo, wakati nchi na taasisi zenye uwezo wa kusambaza chanjo hizo zikibaki kimya.

Dkt. Adeola Fowotade, daktari bingwa wa elimu ya virusi katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Ibadan, Nigeria, amesema wiki kadhaa zilizopita, DRC na Nigeria ziliashiria kuwa ziko tayari kutoa leseni ya chanjo muhimu kuingizwa nchini mwao.

"Hii ni hatua ya kupongezwa katika kusaidia kupunguza kuenea kwa virusi katika nchi za Afrika na ninatumai nchi zingine zitapokea chanjo," anasema.

"Moja ya changamoto tutakayokuwa nayo ni hii ambayo tumekuwa nayo kila wakati wa utoaji wa chanjo barani Afrika - taarifa na habari za uongo na watu kukosa imani, haswa kwa kuwa huu ni mpan-go unaoungwa mkono na serikali." ameeleza Daktari. Huyu.

DRC ina uzoefu wa utoaji wa chanjo kwa kiasi kikubwa kutokana na milipuko wa Ebola - virusi hatari ambavyo vinaweza kusababisha homa ya ghafla, kuchoka, maumivu ya misuli na koo.

Askofu atahadharisha

Askofu Mkuu Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaac Amani, ametoa tahadhari za kiafya dhidi ya ugonjwa huo kwa mapadre, watawa na walei wa jimbo lake.

Amewataka kuanzia sasa, kwenye shughuli zote, ikiwemo ibada na misa mbalimbali, waumini kuepuka kusalimiana kwa mikono wakati wa kutakiana amani kwenye misa na nje ya ibada.

Askofu Amani katika taarifa yake kwa viongozi wake hao wa kanisa kupitia barua yake na kuwataka pia wazingatie kuepuka kukumbatiana, kucheza muziki kwa kugusana, kuweka vitakasa mikono, sabuni na maji tiririka kila mahali, huku akihimiza kwamba kujikinga ni nafuu, kujitibu ni aghali.



Riwaya

Viaticum-5

Sakramenti ya Mwisho



Kwa wasomaji wapya: Hatimaye Eddy ameanza kulainika baada ya ushawishi na sasa anapanga safari, je nini kitaendelea? Tiririka na riwaya hii “tamu sana...”

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

“USIJALI mpenzi wangu, ila usisahau kuja kunia-ga na ukirudi kutoka Mwanza, usisahau kuniletea sato wabichi na dagaa waliokaangwa” Alitania.

“Mbona unaagiza kabisa wakati umesema nije kukuaga? Au hutaki jirani zako wasikie?”

“Naogopa kuwahiwa”

“Tuliza moyo, mimi ni wako” Eddy alimtania

“Poa baadae basi”

“Baadae” Akakata simu. Eddy akaweka simu mezani na kumgeukia Stella.

“Tiketi iko sawa, huyu mtu yuko serious”

“Kwa hiyo utakwenda?”

“Ndiyo, nitakwenda. Nilitaka nithibitishe uha-lali wa tiketi kabla ya kukupa jibu”

“Kama unaogopa kwenda peke yako naweza kukusindikiza bosi wangu,” Stella alisema huku akirembua macho yake makubwa sambamba na tabasamu la kumtoa nyoka pangoni.

“Hapana mama, utanitia wazimu wa mapen-zi. Wewe inabidi ubaki hapa kuhakikisha Mizani linapendeza kama kawaida yake”

“Yaani bosi kila nikikwambia tusafiri wote unanikatalia, kwa nini lakini?” Alilalamika

“We mtoto unaweza kunifanya niuze nyumba yangu kwa hasara kwa ajili yako. Ndiyo maana na-kuogopa”. Eddy alijibu kwa utani huku akicheka.

Akanyanyua zile fedha kutoka mezani, aka-zifunga kwenye karatasi kama zilivyokuwa ali-pozipokea, akazirudisha kwenye bahasha, “chukua hizi fedha pamoja na ujumbe tulioupokea, kavi-fungie kwenye sanduku lako la chuma. Acha zikae humo mpaka nitakaporudi kutoka Mwanza”

“Bosi, mbona unanitisha tena?”

“Ni tahadhari tu. Sitaki tuzitumie hizi fedha mpaka tutakapojua zimetoka wapi, na sababu iliy-omfanya huyu mtu aniite huko Mwanza.”

“Kama mambo yakienda sawa itakuwa kheri, vinginevyo itabidi tumrudishie pesa zake. Tena kama alikuwa akijaribu kunipa rushwa kwa saba-bu yoyote ile, nitamfikisha kwenye vyombo vya dola”

“Sawa bosi, hilo hata mimi naunga mkono,” Stella alijibu kwa furaha. Akainuka kutoka kwenye kiti alichokalia, akajitengeneza vizuri sketi yake kwa kuivuta chini na kuinyoosha sehemu ya nyu-ma kwa viganja vya mikono yake, kisha akain-yanyua ile bahasha.

“Sijui kwa nini kila nikiukumbuka ujumbe tuliousoma, nywele zangu zinanisisimka! Nahisi safari yako itakuwa na mambo mazito yatakay-ofanya Mizani liwe na thamani kubwa kiasi cha kuuzwa kwa dola kama siyo paundi za Kiingereza” Stella aliongea kwa hisia.

“Hata mimi naamini hivyo, tuombe uzima tu”

“Mungu ni mwema atakulinda bosi, maana sisi tunafanya kazi ya kitume japo kwa namna tofauti sana”

“Amen, uko sahihi Stella.”

Bila kuongeza neno, Stella akageuka na kuon-doka taratibu huku akitingisha sehemu ya chini ya kiuno chake.

Kengele ya saa iliyokuwa ikiendelea kugon-ga mfululizo ndiyo iliyomzindua Eddy kutoka kwenye lepe zito la usingizi.

Alipofumbua macho tu akayatupa moja kwa

Inaendelea Uk. 29



Viaticum-5

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

moja mahali alipoiweka saa hiyo. Japokuwa chumba kilikuwa na mwanga hafifu, aliweza kusoma majira bila tatizo.

Ilikuwa imeshatimia saa kumi na moja na robo alfajiri. Akainyanyua, akazima kengele kisha akairudisha mahali ilipokuwa.

Saa hii aina ya Omega alipewa na rafiki yake mmoja raia wa Uganda, miezi nane iliyopita, alipokwenda huko kwa shughuli maalum.

Kwa bahati mbaya rafiki yake huyo aliuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana mwezi mmoja tu baadae.

Tangu wakati huo amekuwa akiitunza saa hii kwa ukumbusho na kuivaa mara chache tu anapokwenda kwenye shughuli maalum.

Baada ya kuweka saa pembeni akanyanyua simu yake ya mkononi, akaangalia kama kuna ujumbe wowote ulioingia.

Zaidi ya jumbe ishirini zilikuwa zimeingia, lakini hakukuwa na ujumbe wowote unaohitaji kushughulikiwa haraka.

Akaweka simu pembeni. Akateremka kutoka kitandani, akatembea hadi pembeni ya chumba mahali lilipo kabati dogo lililojengewa ukutani.

Akatoa sanduku lake, akalifungua, akachukua mfuko mdogo wa plastiki aliohifadhi nguo zake za kufanyia mazoezi ya karate, wenyewe huziita Gi. Akazivaa, na kujifunga mkanda kiunoni mwake.

Ilikuwa kawaida ya Eddy kufanya mazoezi ya karate kila siku alfajiri, kabla ya kuoga na kuanza pilikapilika za siku. Tabia hiyo ilimsaidia sana kulinda heshima ya mkanda mweusi wa Goju-ryu alioupata miaka mingi iliyopita.

Eddy alizingatia sana utaratibu huu aliofundishwa na sensei wake tangu alipoanza mafunzo akiwa na mkanda mweupe.

Sensei huyo alimwambia “mafunzo haya na mwisho. Siku utakayoacha mazoezi na ujuzi ulioupata, nao utakuacha taratibu.”

Maneno hayo yalimkaa vyema kichwani



kwake, na ndiyo hasa yaliyomtia moyo kuendelea na mafunzo hadi kufikia daraja la mkanda mweusi dani (degree) ya nne.

Baada ya kuweka kila kitu sawa ndipo alipogundua tatizo lililomkabili. Chumba kilikuwa kidogo kuliko kilivyokuwa kikionekana.

Hii lilisababishwa na jinsi samani zilivyokuwa zimepangwa ndani humo. Likamjia wazo la kwenenda kufanyia mazoezi nje, lakini akaona haitakuwa busara kwani hakuwa nyumbani kwake; bali kwenye moja ya hoteli maarufu mjini Mwanza.

Aliwasili mjini hapa saa kumi na moja jioni ya siku iliyotangulia, kwa ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania. Ndege hiyo iliondoka Dar es Salaam saa kumi jioni.

Kwa vile hakuwa na mwenyeji wa kumpokea uwanja wa ndege, akachukua taksi iliyomleta kwenye hoteli hii iliyoko eneo la Kapripointi.

Baada ya kumteremsha, dereva huyo aliyejitambulisha kwa jina la Frank alimpa namba yake ya simu na kumuomba amtafute muda wowote atakapohitaji usafiri.

Kwa vile Eddy hakuwa na safari yoyote jioni hiyo, akamwambia amfuata kesho yake saa kumi na mbili na nusu asubuhi, kumpeleka Kanisa Kuu la Epifania lililoko eneo la Bugando, karibu na Hospitali ya Rufaa Bugando.

Baada ya kufikiri kwa sekunde chache, Eddy akaona hana sababu ya kwenda nje, au kuahirisha ratiba ya mazoezi kwa sababu ya udogo wa chumba.

Akaamua kufanya mazoezi ya viungo kwa wa nusu saa, akakaa kwenye tafakari (meditation) kwa robo saa, kisha akainuka kucheza kata iitwayo sanchin. Alipomaliza kata hiyo akajinyoosha viungo tena ndipo akaingia bafuni kuoga.

Itaendelea wiki ijayo...

Ubelgiji kuongeza nguvu nishati safi ya kupikia

Na Mwandishi WETU

TANZANIA na Ubelgiji zimekubaliana kushirikiana katika sekta ya nishati, hususan matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Ushirikiano huu ni sehemu ya kuharakisha mkakati wa miaka 10 ambao unataka kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati hiyo.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika mazungumzo baina ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko, ambaye aliongoza ujumbe wa Tanzania na Waziri wa Nishati wa Ubelgiji, Tinne Van Straeten, kwenye kikao maalumu kilichofanyika mjini Windhoek, Namibia wiki iliyopita.

Kikao hicho kilifanyika kandoni mwa mkutano wa Mkutano wa Nchi za Afrika kujadili matumizi ya Haidrojeni katika kuzalisha umeme.

Katika kikao hicho, viongozi hao wawili walikubaliana kushirikiana kutekeleza kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa maendeleo ya Afrika.

“Mheshimiwa waziri kama ulivyosikia, Tanzania inaendesha kampeni maalumu ya nishati safi ya kupikia kwa Tanzania, Afrika na kimataifa chini ya usimamizi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa msingi huo tunasimamia utekelezaji wa mpango maalumu wa miaka 10 ulioanza mwaka huu hadi mwaka 2030 ambapo tunatarajia asilimia 80 ya Watanzania wawe na uwezo wa kutumia nishati safi ya kupikia...”

“Kwa maana hiyo, ninachukua fursa hii kuwaomba Serikali ya Ubelgiji itusaidie katika kuhakikisha tunakamilisha kikamilifu mpango huu wa kitaifa...”

“Tungetamani kuungwa mkono na Ubelgiji katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kama ambavyo imekuwa ikifafanya katika sekta



**Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,
Dkt. Doto Biteko**

nyingine ikiwemo elimu na uwezeshaji katika masuala ya usawa kijinsia,” Dkt. Biteko alimweleza Waziri Straeten.

Aliongeza kuwa katika sekta ya nishati ambayo ndiyo hasa iliyowakutanisha kwenye mkutano huo, ni msingi wa mkakati wa maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji kwa uchumi wa Tanzania, ikiainishwa kwamba inasidia kuimarisha hali za maisha ya watu.

Dkt. Biteko alieleza kuwa anatambua changamoto zinazolikabili taifa kwenye sekta hii ya nishati ni muhimu kushughulikiwa kwa wakati ikiwemo kuongeza uwezo, kuboresha miundombinu, kujenga uwezo zaidi wa kuwa na vyanzo vingi vya nishati mbadala.

Dkt. Biteko alisema anaamini kupitia ushirikiano na kushirikishana kwa kubadilishana uzoefu katika changamoto zinazoikabili sekta ya nishati wataweza kukabili vyema changamoto hizo, hivyo Tanzania imefungua milango na inatoa fursa kwa wawekezaji kutoka Ubelgiji, katika sekta ya nishati kuwekeza nchini.

Waziri huyo wa Ubelgiji, Straeten, alisema nchi yake iko tayari kuunga mkono jitihada za matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwa ni mkakati wa kimataifa wa uhifadhi wa mazingira na kuwawezesha wananchi kukuza mapato na maendeleo ya kiuchumi.

Na Hellen
NGOROMERA

Uhusiano



Kinachokera wanaume wengi kwenye uhusiano - 2

WIKI iliyopita nilizungumza mambo yanayowakera wanaume ambayo hufanyiwa na wake au wapenzi wao, na leo nitaendelea na sehemu ya pili ya mada hiyo.

Mara kadhaa wanandoa wanavurugana kutokana na jinsi ambavyo mmoja wao anawachukulia ndugu, wakiwamo wazazi wa upande wa pili.

Hali ya mmoja kutoelewana na ndugu au wazazi wa upande mwingine, hutokea kwa mwanamke na mwanamume, ingawa mara nyingi hili ni tatizo la wanawake walio katika ndoa.

Hali inakuwa mbaya zaidi pale mmoja anapoamua kuishi na wazazi au ndugu wengine ambao mwenza wake haelewani nao.

Hili husababisha mtihani mkubwa kwa yule mwenye wazazi. Mtihani unakuwa kwake kuchagua aambatane na nani kati ya mwenza au wazazi.

Kama akiendelea kuishi na wazazi wake, anaweza kusababisha ndoa yake kutetereka na hata kuvunjika.

Iwapo atachagua kuwarudisha wazazi wake kijijini, ataiumiza nafsi yake kwani mpango wake ulikuwa ni kuona wazazi wake wakiishi kwa raha wakiwa karibu naye.

Kuna wale ambao wasipowapenda ndugu au wazazi wa mwenza wake husema wazi.

Ukikutana na mtu wa aina hiyo, hali inaweza isiwe mbaya sana kwa sababu mnaweza kuyazungumza mambo kwa uwazi.

Lakini, wapo wengine ambao huonyesha chuki zao dhidi ya ndugu wa wenza kwa siri, kwa kufanya vituko ambavyo havionyeshi waziwazi kuwa ana chuki dhidi yao.

Hapa hali huenda ikawa mbaya sana kwa sababu mwenza anaweza kuendelea kuishi na ndugu zake akidhani kuwa hali ni shwari, kumbe kuna visa na mikasa inayoendelea chinichini bila ya yeye kuwa na habari.

Unakuta mpaka hali inapokuwa mbaya zaidi ndipo hugundua na aghalabu katika hatua hiyo, inakuwa ni vigumu sana kuchukua hatua ambazo zinaweza kurekebisha hali.

Ni vyema basi, mwanamke unapoamua kuolewa, afahamu kuwa familia ya mumeo ni sehemu ya familia yako, hivyo unalazimika kuwapenda ndugu wa mume kama ndugu zako na hali hiyohiyo kwa mwanamume.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen-2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.



Mitindo & Urembo

Vazi la kitenge lina thamani yake

KITENGE hakijawahi kuisha thamani kwa miongo mingi sasa na kimeendelea kuwa utambulisho kama vazi kutoka Bara la Afrika.

Kuvaa kitenge kuna-tosha kukuelezea kuwa wewe ni mpenda utamaduni wa Kiafrika, hasa kwa kipindi hiki ambacho mitindo mingi inayovaliwa ni ile ya nchi za magharibi.

Kitenge kinaweza kutumika kushona vazi la aina yoyote na likapendeza. Kitenge kinatumika kushona gauni, shati, kaptula, suruali, nguo za shughuli kama harusi, send off, sherehe za jikoni na kadhalika.

Dondoo muhimu

*Rangi yako; hapa kabla hujanunua jaribu kupata ushauri wa kitenge kitakachoendana na rangi ya mwili wako.

*Umbo lako; fundi pamoja na wewe mwenyewe mshauriane kuhusu mshono unaoitaka ikiwa ni shati, gauni, suruali.

Ikiwa wewe ni mnene epuka rangi zinazong'aa.

*Kama umeshona gauni fupi au refu linalofanya kiutu kionekane, jaribu kuvaa viatu virefu vinavyoweza kuonekana kwa urahisi.

Unaweza kuangalia moja ya rangi zilizoko kwenye kitenge chako ukavaa kiutu cha rangi hizo. Kiutu cha kufunika ni bora zaidi.

Na Agatha Charles



Ondoa weusi kwa maziwa, manjano

SHEMU kama kwapa na katikati ya mapaja ndizo zinaongoza kwa kuwa na weusi.

Wapo pia ambao hupata weusi katika sehemu tofauti kama chini ya macho, nyuma ya magoti na maeneo mengine ya mwili.

Leo nimekuwekea namna bora ya kuondoa hali hiyo kwa kutumia maziwa 'fresh' na manjano.

Maziwa yana sifa ya kung'arisha ngozi na manjano husafisha ngozi.

*Chukua maziwa vijiko viwili na unga wa manjano kiasi cha kutengeneza uji mzito wa mchanganyiko huo, kisha pakaa sehemu iliyoathirika na weusi.

Tumia pamba au kitambaa laini kusugue taratibu eneo husika, baada ya muda kidogo nawa na endelea na huu utaratibu kila siku unapopata muda. Hakika utapata matokeo mazuri baada ya muda.
Kwa maoni na ushauri: piga simu 0656531217

Afcon



Iwe shamba darasa kwa mataifa yetu

Na John MARWA

KANDANDA ndio mchezo maarufu zaidi duniani ambao umekuwa chanzo kikuu cha furaha kwa binadamu wengi wenye tamaduni, lugha na asili tofauti, lakini wameunganishwa na sayansi ya soka.

Ndio maana mataifa matatu ya Tanzania, Kenya na Uganda yanafanya kila linaloweze kana kuhakikisha Afrika na dunia inafurahi ifikapo 2027 nchi hizo zitakapokuwa wenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika - 'Pamoja Afcon 2027'.

Kila mwana Afrika Mashariki, mpenda kabumbu anamuomba Mungu apate uzima na macho kushuhudia historia ikiandikwa na yeye akiwa sehemu ya wino utakaotumika kuthibitisha hilo.

Pamoja na kuwa soka limekuwa kivutio kikubwa zaidi, wapo waliobeba tamu na chungu ya kilele cha furaha yake, hawa siyo wengine bali ni walimu, makocha ama wakufunzi na wataalamu wa michezo, hawa ndio hutafsiri picha ya kabumbu katika kila dakika 90.

Msingi wa jambo lolote huandaliwa kuanzia kwenye chanzo na chanzo cha vipaji vingi vya soka, huanzia kupikwa vingali vidogo.

Soka linawahitaji vijana wadogo 'kumezeshwa' na kutengenezwa kwenye misingi ya sayansi ya soka la kisasa.

Licha ya kila jitihada zinazofanywa na serikali zote tatu kuyaendea mashinadano hayo, je ni kwa kiwango gani tunatumia michano hiyo kama fursa ya kuzalisha makocha bora na wa kisasa katika kuibua na kukuza vijana ambao watakuwa mradi wa kuienzi Pamoja Afcon 2027?

Huko kwenye nchi zinazoabudu soka, tumewahi kusikia 'Class of 1998' pale Manchester United. Huo ni mfanano tu kati ya mingi ambayo ilitumika kama shamba darasa la kuzalisha nyota na wahafidhina wa mchezo wenyewe kwa taasisi ama taifa.

Ndipo hapa napowaza kwa sauti - kwanini tusiwe na 'Class of 2027' katika ngazi ya makocha, wataalamu wa michezo na wachezaji nyota vijana ambao watabaki kuwa alama ya miaka mingi ya mafanikio na faida za kuwa wenyeji?

Tunahitaji kuwapa elimu na kuwawezesha vijana kubobea katika maarifa ya kabumbu kwa kutumia fursa za kuwa wenyeji wa michuano hiyo ya Afcon.

Ni wazi tunahitaji miundombinu ya viwanja bora vya kuchezea na kufanyia mazoezi, lakini tunawaza tukiwa na hiyo miundombinu bora bila kuwa na matumizi nayo bora, itatusaidia nini?

Kumbe tunahitaji kuwa na miundombinu bora, tunahitaji kuwa na walimu, makocha na wataalamu wa masuala ya soka ili waweze kuitumia hiyo miundombinu kupanda, kupalilia na kuvuna mavuno yaliyo nona kwa maslahi mapana ya mataifa yote.

Tusifurahie tu kuwa wenyeji, tusifurahie tu kujenga viwanja na miundombinu mingine, lakini kama wahafidhina wa kabumbu, tujivunie zaidi Pamoja Afcon 2027 kutuachia wataalamu, makocha na shamba darasa la mavuno ya 'Class of 2027'.



Rich Mavoko afunguka kuhusu WCB



Dar es Salaam, Tanzania

MSANII wa bongo fleva Richard Martin 'Rich Mavoko' amegoma kuzungumzia kebo yake ya zamani ya WCB kwa madai kwamba hataki kuonekana kama bado anaitamani.

Rich alisema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa na mtangazaji wa chombo kimoja cha burudani cha jijini hapa aliyemtaka kuzungumzia kuhusu kutolipa lebo hiyo chochote wakati anaondoka kama walivyofanya wenzake akina Harmonize na Rayvanny.

Alibainisha kuwa, "Mimi nafikiri nimeshaongelea sana hiyo lebo, sijui miaka mingapi tangu nimetoka, kwaiyo kwangu kuiongelea ni sawa na

kumuongelea mwanamke ambaye umeshaachana naye hivyo itaonekana kama bado unampenda.

Aliongeza kuwa, "Ukisema sijalipa chochote na mimi nitakwambia na mimi pia sijalipwa chochote. Hii ndo maana nimekwambia sipendi sana kuzungumzia hayo mambo ila ukitaka tuongee 'fact' nitakuwa 'fact' na wewe nitakutaka unipe 'fact'."

"...Usiingilie mkataba hicho ni kitu cha siri hivyo sipendi kukiweka hadharani hata mimi nitakuwa najifunga, najua hayo mambo yamepita ila nataka ujue mkataba ni siri. Ili upate kitu kizuri, nenda kwa kiongozi wa lebo, kwa upande wangu hii ishuru nimeshaongea sana," alimalizia.

Selena Gomez awa bilionea mdogo zaidi

Grand Prairie, Texas, MAREKANI

INAWEZEKANA hivi ndivyo unavyoweza kusema kwa msanii huyu wa Pop na R&B kutoka Marekani Selena Gomez Sasa rasmi ameifikia hadhi ya kutambulika kama bilionea.

Selena amefanikiwa akiwa na miaka 32 pekee akiwa miongoni mwa wasichana wadogo nchini humo amefikia hadhi hiyo.

Gomez ana miliki utajiri wa dola za Marekani billioni 1.3 zaidi ya Sh. trilioni 3.5 huku sehemu kubwa ya utajiri wake ukitokana na bidhaa zake za urembo za Kampuni ya 'Rare Beauty Empire' ilianzishwa miaka mitano iliyopita.

Siri kifo cha Rich Homie hadharani

Atlanta, Georgia, MAREKANI

SIRI ya kifo cha rapa wa Marekani Rich Homie Quan (34), ambaye wiki iliyopita taarifa za kifo chake zilienea duniani, sasa ni wazi kuwa amefariki kwa kuzidisha matumizi ya dawa za kulevya (drug overdose).

Kwa mujibu wa mpenzi wa marehemu, aliwaambia polisi kwamba siku ya tukio, alimkuta amelala kwenye kochi asubuhi, sehemu ambayo alikuwa amekaa tangu usiku baada ya kutumia dawa hizo. Baada ya kumkuta akidhani amelala, alimfunika na blanketi na kisha akaendelea na mchakato wa kumpeleka mtoto wao shuleni. Wakati anarudi nyumbani, alimkuta bado akiwa amelala ndipo akajaribu kumuangalia na kugundua kuwa hapumui huku damu, zikimtoka puani na mapovu mdomoni



Kiungo mkabaji wa Simba, Yusuf Kagoma

Ya akina Kagoma hajulikani mwema wala muovu

Na John MARWA

SIYO kwamba nyakati haziendi, siyo kwamba ya kale hayanuki, ila muda ni mwalimu mzuri na uzoefu ni mkufunzi wa madarasa yote.

Katika dirisha kubwa la usajili wa wachezaji Tanzania, kuna mengi yameibuka na kutukum-busha ya Mbuyu Twite na machozi ya Aden Rage, tukayaona ya Morisson, tukayaishi ya Feisal na Dube, lakini msimu huu tuna shindwa kuamini tunayosikia, maana yanamalizika kiaina.

Ni soka letu, kivyetu vyetu, ndio maana songombigo haziishi kwani ndio chakula cha mataikuni wa soka la Bongo; Simba na Yanga. Stori kama hizo ni aghalabu kuzisikia kwa klabu nyingine nje ya Kulwa na Doto hao wa Dar es Salaam.

Mchezaji kusaini kandarasi mbili kwa wakati mmoja ni hadithi za karne ya 18, lakini bado Tanzania tunaishi nazo kama hadidu rejea kila wakati.

Waswahili walisema biashara haigombi, lakini kwanini biashara ya wachezaji wa Bongo ni vita ya majimaji? Haimalizikagi salama, licha ya kuwa ligi yetu inatajwa kushika nafasi ya sita kwa ubora Afrika.

Msimu huu Simba SC katika usajili wake wote wa wachezaji wa ndani, umeingia dosari licha ya kuwa kwa asilimia zote wachezaji wako upande wao.

Lameck Lawi kutoka Coastal Union, ndiyo pekee hayuko pale Uwanja wa timu hiyo ya Mtaa wa Mimbazi, Mbweni, Dar es Salaam.

Wachezaji Mashaka Vaentino kutoka Geita, Yusuph Kagoma kutoka Singida, Awesu Awesu kutoka KMC FC, nao kelele ni nyingi zilizikika vilio bila machozi.

Lakini pia Simba akamruhusu Israel Mwenenda kuondoka bila vurugu, ingawa vita vyake na Singida Black Stars nayo imepamba moto, hii tuiweke kando.

Haya ya Kagoma, Awesu, Lawi, Mashaka ndio yale ya Twite, Fisal, Dube na Morrison kwa miaka ya hivi karibuni na yote, Simba na Yanga wanahusika ama mmoja wao.

Tulipofika ni kwa sababu ya “cha kichwa kitamu, na cha mkia kitamu”, licha ya kuwa ni ukweli uliowazi kuwa Simba na Yanga ni zaidi ya klabu za mpira nchini, lakini kuna wanaohalalisha uovu wao.

Ukilitazama sakata la Kagoma ni ukwel uliowazi kuwa kuna mkono unaotumika kulamba asali pande zote, ama unashinikizwa kulamba asali upande mmoja na kuukomoa upande mwingine.

Biashara ya mchezaji ilifanywa na waajiri wake Singida Fountain Gate kwenda Simba licha ya kuwapo makubaliano na Yanga kabla ya hapo ambayo hayakukamilika.

Mchezaji amepewa kibali na leseni ya kukitwanga unyamani, leo taasisi iliyompa kibali inadaaiwa kumsimamisha?

Kamati ya sheria na hadhi za wachezaji chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) inathibitisha kuwa ‘chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba’- hapo ndipo kuna utakatishaji biashara ya wachezaji wazawa.

Kama ni kuanguka katika eneo hili, basi tulikwisha lala usingizi wa pono, huku tukiziishi ndoto za mchana tukijidhanja tumesimama.

Kukosa weledi, roho mbaya na vita vya Pwagu na Pwaguzi ndio inaturejesha huku kila nyakati.

MICHEZO

Jumatatu, Septemba 9-15, 2024



Tanzania vs Guinea ndani mtiti, nje mtiti

Na John MARWA

TAYARI Kikosi cha Timu ya Soka ya Tanzania; Taifa Stars kimewasili Abidjan, Ivory Coast kwa mchezo wake wa pili wa Kundi H, kufuzu michuano mikubwa ya kabumbu Afrika (Afcon) kwa mwaka 2025, dhidi ya Guinea utakaochezwa kesho, Septemba 10.

Taifa Stars inauendea mchezo huo ikiwa na hisia chanya za kusaka pointi tatu muhimu ikiwa ni mara baada ya kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza dhidi ya Ethiopia uliopigwa Septemba 4 kwenye Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ni mchezo mgumu zaidi ya uliopita kwa Stars, huku Guinea ikiutazama kama sehemu ya kuvuna alama tatu mara baada ya kupoteza mchezo wao wa kwanza dhidi ya DR Congo kwa bao moja kwa bila wakiwa ugenini nchini Congo.

Guinea hawakupoteza kwa aibu kutokana na

ubora waliouonyesha na uimara wa kikosi chao ambacho kinaundwa na nyota wengi wanaosakata kabumbu barani Ulaya wakiwamo Naby Keita, Mohamed Bayo, Amadou Diawara na wengine wengi.

Dakika 90 zijazo kwa mataifa yote mawili hazina ajizi, ni kufa ama kupona, kwani timu itakayokubali kupoteza, basi itakuwa imejiweka kwenye mazingira magumu ya kupata tiketi ya kuelekea kwenye fainali za Afcon 2025, nchini Morocco.

Guinea wameonyesha uimara wao dhidi ya DR Congo licha ya kupoteza, ni timu ambayo 'imekalimika kila idara.' Hawa wana uzoefu mkubwa na ukomavu wa kuamua aina ya michezo kama huu dhidi ya Taifa Stars.

Shaka ya Watanzania ni aina ya kikosi ambacho Kocha Hemed Morocco aliikita na kukiamini, chenye mseto wa vijana ambao walishindwa kuonyesha kile ambacho watu walihitaji kwenye mchezo dhidi ya Ethiopia.

Taifa Stars inapaswa kuamka na kujipanga kwa haraka, hasa katika eneo la kiungo cha ushambuliji na eneo la ushambuliaji, ni maeneo ambayo yalizerota sana kwenye mchezo uliopita. Kasi, maarifa na ubunifu ni eneo adhimu la kuimarishwa kabla ya kuwavaa Guinea.

Licha ya kuuhitaji mchezo, bado Stars inapaswa kuingia kwa tahadhari kubwa kwa maana wanaenda kukutana na timu ambayo iko bora katika idara zote uwanjani.

Pamoja na kutazama maeneo ya kuimarishwa, bado Taifa Stars inahitajika kuungwa mkono zaidi na Watanzania na kuhimiza wananchi kuitazama kesho na kujadili wapi kunahitaji maboresho zaidi ili kupata matokeo mazuri ya kuwezesha timu kusonga mbele.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

